Uelekeo
Leo yetu ndiyo kesho yetu
UMG Kasi na Ubora
| ISSN 2953-2787 | Toleo Na. 00078 | Bei Tanzania sh 1,000 | Jumatano Agosti 14-20, 2024 |

**Homa ya Nyani:** Kwa nini Mpox inaenea kwa kasi Afrika Mashariki na Kati? Uk. 7&8

**Mwana-CCM ajitosa kuwania Ubunge EALA** Uk. 2



**Zima zote washa kijani inavyopukutisha wapinzani kila kona** Uk. 12



**Chatanda: Wazazi waacheni watoto wa kike wasome** Uk. 14



**Wanaodhalilisha walimu 'walimwa' kadi ya njano** Uk. 8



Katika kipindi changu hiki, sitegemei kuona mwalimu akinyanyaswa, akionewa...

## Dk. Mpango: EAC itumie vema idadi kubwa ya vijana Uk. 4



## Mwanafunzi 'anusa' kifo simu ikilipuka chumbani kwake Dar Uk. 5



# Samia aipaisha Hospitali ya Rufaa Mkoa Temeke Uk. 4

- **Huduma ya usafishaji damu wagonjwa wa figo yazinduliwa**




**Kimataifa** Ukraine yadhibiti km 1,000 za mraba ndani ya Urusi katika miaka miwili Uk.19

# Mwenge wazindua Jengo la Wagonjwa wa Dharura Shinyanga

**Na Mwandishi Wetu**

KIONGOZI wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa, Geofrey Mnzava, ameridhia kuzindua jengo la kutolea huduma za dharura (EMD) katika Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga baada ya kujiridhisha na utekelezaji wake.

Jengo hilo lilipo katika Kijiji cha Iselamagazi, lilizinduliwa juzi.

Akisoma taarifa ya mradi kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, Dk. Nuru Yunge, alisema ujenzi wa jengo hilo umegharimu Sh. Milioni 300 ambazo ni za UVIKO zilizotolewa na Serikali Kuu.

Jengo la wagonjwa wa dharura lilianza kutumika Februari 28, mwa huu.likiwa msaada mkubwa kwa kutatua kero kwa wakazi wa halmashauri hiyo ambao walikuwa wakitembea umbali mrefu wa zaidi ya kilomita 40 kupata huduma katika Manispaa ya Halmashauri ya Shinyanga.

Ujenzi wa jengo hilo ulianza mwaka wa fedha 2022/2023 na kukamilika mwaka wa fedha 2023/2024.

Wakizungumza kwa wakati tofauti, baadhi ya wakazi wa Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, walimshukuru Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, kwa kuendelea kuboresha huduma za afya katika Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga.

Kauli mbiu ya Mbio za Mwenge wa Uhuru kwa mwaa huu ni Tunza Mazingira na Shiriki Uchaguzi wa Serikali za Mitaa kwa Taifa Endelevu.




# Mwana-CCM ajitosa kuwania Ubunge EALA



Grace akikabidhiwa fomu ya kuwania Ubunge EALA jijini Dar es Salaam jana.

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU Mwenyekiti wa Taasisi ya Mwalimu Nyerere Mkoa wa Kilimanjaro, Grace Saulo Mali, amechukua fomu ya kuomba ridhaa ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), kuwania Ubunge wa Bunge la Afrika Mashariki.(EALA)

Kada huyo wa CCM ambaye kitaaluma ni mwalimu, alichukua fomu hiyo katika Ofisi Ndogo za Makao Makuu ya Chama, Mtaa wa Lumumba, jijini Dar es Salaam jana.

Akizungungumza na waandishi wa habari baada ya kuchukua fomu hiyo, Grace alisema ana dhamira ya dhati ya kuwania kiti hicho kilichoachwa wazi na aliyekuwa Mbunge wa Bunge la Afrika Mashariki, Dk.Shogo Mlozi, aliyefariki dunia Juni, mwaka huu.

Grace alimshukuru Mwenyekiti wa CCM, Rais Dk.Samia Suluhu Hassan na Chama kwa kuweka utaratibu mzuri wa kuwania nafasi hiyo.

Alisema kipaumbele chake kikubwa akifanikiwa kupata nafasi hiyo ya kuliwakilisha Taifa katika Bunge la Afrika Mashariki kitakuwa ni elimu.

"Pia kuwasaidia vijana waliosoma, lakini hawana ajira kwa kuwaunganisha na fursa," alisema.

Aliwataka Watanzania kumuunga mkono Rais Dk. Samia katika sekta mbalimbali alizowekeza.

"Tumuunge mkono Rais katika sekta ambazo amewekeza kwa ukubwa," alisema.

CCM ilianza juzi kutoa fomu hizo nchini kote.

> **Ninamshukuru Mwenyekiti wa CCM, Rais Dk.Samia Suluhu Hassan na Chama kwa kuweka utaratibu mzuri wa kuwania nafasi hiyo.**

# Wananchi 4,870 wapata huduma ya ultrasound Songwe



**Na Mwandishi Wetu, Songwe**

TAKRIBANI wananchi 4,870, wamepatiwa huduma za Ultrasound ikiwemo wajawazito katika Hospitali ya Wilaya ya Songwe.

Hiyo ni miaka mitatu tangu kuanza rasmi kutoa huduma kwa hospitali hiyo hali iliyopunguza rufaa kwa wagonjwa.

Hayo yalibainishwa na Mganga Mfawidhi wa hospitali hiyo, Dk. Ntufye Kapesa, wakati akielezea hali ya utoaji wa huduma za matibabu kwenye hospitali hiyo.

# Serikali iungwe mkono kukabili changamoto za kiuhifadhi

**Na Wemael Mmaraba**

WANANCHI wamehimizwa kuunga mkono serikali katika juhudi zake za kukabiliana na changamoto za kiuhifadhi zinazoweza kusababisha hatari ya kupungua kwa tembo.

Mkurugenzi wa Taasisi ya Kudhibiti Uhalifu Mtandaoni, Shubert Mwarabu, alitoa wito huo katika taarifa yake kwa Siku ya Tembo Duniani inayoadhimishwa Agosti 12 ya kila mwaka.

Alisema kutokana na baadhi ya nchi za mashariki ya mbali kufunga masoko ya biashara ya meno ya tembo iliyoshamiri kwa asilimia 75 ya masoko yote ya meno ya tembo, wahalifu sasa wanatumia mitandao ya kijamii kufanikisha ujangili na biashara hiyo.

Alisema tembo wamekuwa wakiuawa kwa lengo la kupata meno, ujangili ambao unapaswa kupigwa vita.


Alisema kuwepo na masuluhisho ya migogoro baina ya binadamu na tembo kwa kuweka njia rafiki za kudhibiti migogoro hiyo ikiwemo mizinga ya nyuki na njia nyinginezo.

Aidha, alitoa wito kwa wananchi kutoingilia maeneo ya hifadhi kwani kufanya hivyo husababisha uharibifu wa hifadhi ambazo ni makazi ya kudumu ya tembo na wanyama wengine.

Alitaja baadhi ya bidhaa za wanyamapori ambazo zimekuwa zikiuzwa mitandaoni kuwa ni meno ya tembo, magamba ya kakakuona, pembe za faru na hata wanyama hai kama chui ambao hufugwa majumbani katika baadhi ya nchi za Uarabuni.

Mkataba wa CITES unaoratibu biashara ya viumbe vilivyo hatarini kutoweka vya wanyama na mimea, unazuia biashara ya viumbe vilivyo hatarini zaidi kutoweka, lakini uwepo wa biashara hiyo kwenye mtandao wa intaneti kunaleta ugumu kudhibiti biashara hiyo.

**Alitaja baadhi ya bidhaa za wanyamapori ambazo zimekuwa zikiuzwa mitandaoni kuwa ni meno ya tembo, magamba ya kakakuona, pembe za faru na hata wanyama hai kama chui ambao hufugwa majumbani katika baadhi ya nchi za Uarabuni.**



# Kesi wizi wa fedha za Hekalu yaahirishwa

**Racheal Mayanga Na Hidaya Machupa**

KESI ya wizi wa fedha Sh. 19,415,000 mali ya Hekalu la Shree Sanatan Dharma Sabh jijini Dar es Salaam inayowabili Vascant Solanki (73) na Ramsishchanra Shah (62) imeahirishwa mahakamani baada ya wakili wa mshtakiwa kutoa udhuru.

Kesi hiyo ilitakiwa kuanza usikilizwaji katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, lakini Wakili Richard Rweyongeza anayemtetea mshtakiwa wa kwanza alitoa udhuru wa kutohudhuria kesi hiyo kwa kuwa alikwenda kuhudhuria vikao vya awali vya uhujumu uchumi.

Wakili wa Serikali, Grace Mwanga, alithibitisha mbele ya Hakimu Mkuu wa mahakama hiyo, Aaron Lyamuya, kuwa kesi hiyo ilikuja kwa usikilizwaji.

Awali, ilidaiwa na Wakili Grace kuwa kati ya Januari, 2016 na Novemba, 2016, mkoani Dar es Salaam, washtakiwa hao waliiba Sh. 19,415,000 mali ya Hekalu la Shree Sanatan Dharma Sabh.

Wakili wa mshtakiwa wa pili, Rehema Samwel, aliiomba mahakama kuahirisha kesi hiyo, ombi lililokubaliwa na Hakimu Lyamuya na kuiahirisha hadi Septemba 3, mwaka huu.

Alimtaka shahidi Faustine Mashauri na washtakiwa wote wawili, kuwepo mahakamani bila kukosa wakati wa kusikiliza kesi hiyo.

# ‘Makundi maalum yawezeshwe kufikia miundombinu kidigitali’

**Na Mwandishi Wetu**

ASASI za kiraia nchini kupitia Shirika la The Foundation for Civil Society (FCS), zimeiomba serikali kuhakikisha makundi maalum yanawezeshwa kufikia miundombinu ya kidigitali ili washiriki katika michakato ya maendeleo na kujiimarisha kiuchumi.

Meneja Programu wa FCS, Nasim Losai, alisema hayo katika mkutano wa kitaifa wa watu wenye ulemavu, madiwani na wadau, uliofanyika jijini Dar es Salaam juzi.

Alisema mkutano huo unaangazia ushiriki wa watu wenye ulemavu katika maendeleo, uchumi na kijamii, huku ukiangalia matumizi ya takwimu za sensa katika kuboresha mipango ya halmashauri za wilaya na ngazi za kata.

Aidha, alisema kuwa serikali imekuwa sikivu katika kuhakikisha makundi maalum yanafikiwa na kuwezeshwa katika shughuli za kiuchumi na kujiongezea kipato.

“FCS tuna zaidi ya miaka 20, tumekuwa tukiisaidia serikali hasa katika shughuli za jamii na kutetea watu wenye ulemavu na michakato ya kiserikali, hasa kwenye majengo mengi miundombinu imebadilika na kazi kubwa imefanywa na FCS pamoja na makundi haya,” alisema.



**Meneja Programu wa FCS, Nasim Losai akizungumza na waandishi wa Habari katika mkutano wa kitaifa wa watu wenye ulemavu, madiwani na wadau, uliofanyika Jijini Dar es Salaam.**

Kwa upande wake, mshauri wa kitalamu wa masuala ya watu wenye ulemavu Tanzania, Peter Charlse, alisema malengo ya mkutano huo ni kuwajengea uelewa watu wenye ulemavu katika masuala mbalimbali na kuangazia zaidi eneo la uchumi na kuona fursa zipi walemavu wameweza kushirikishwa na ambazo wanaziweza.

“Ushirikishwaji wa watu wenye ulemavu bado ni mdogo, ndiyo maana, tumewaalika madiwani ili kuangalia changamoto zilizopo na kuwajengea uwezo ili kuyaingiza katika mipango yao ya maendeleo kupitia mabaraza yao ndani ya halmashauri,” alisema.

Naye Mwenyekiti wa Chama cha Walemavu Tanzania, Hamad Abdallah Komboza, alisema changamoto kubwa kwa watu wenye ulemavu ni masuala ya ajira, huku akimuomba Kamshina wa Kazi na vyama vyenye ulemavu kufanya ukaguzi kwenye mashirika na taasisi ambazo zinapaswa kuajiri watu wenye ulemavu, lakini bado hazijatekeleza na kwamba msukumo zaidi unahitajika.

# Samia aipaisha Hospitali ya Rufaa Mkoa Temeke

**Na Mwandishi Wetu**

MABORESHO makubwa yaliyofanywa na Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Temeke (TRRH), yamefanikisha kuzindua rasmi jengo la Huduma za Usafishaji Damu kwa wagonjwa wa figo.

Mkuu wa Wilaya ya Temeke, Sixtus Mapunda, alizindua jengo hilo juzi kwa niaba ya Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu.

Mapunda alisema jengo hilo jipya la usafishaji damu, ni moja ya maboresho makubwa yaliyofanyika hospitalini hapo.

Alisema huduma zitakazotolewa katika jengo hilo zitarahisisha upatikanaji wa huduma za usafishaji damu kwa wananchi wanaoishi maeneo ya karibu na Temeke, hivyo kupunguza changamoto za kusafiri umbali mrefu kutafuta huduma hiyo.

Aidha, akitoa salamu za Waziri Ummy, Mapunda aliwataka wananchi kujenga tabia ya kufanya mazoezi na kuzingatia ulaji bora wa vyakula ili kuepuka magonjwa yasiyo ya kuambukiza kama vile kisukari, shinikizo la damu na matatizo ya afya ya akili, ambayo yamekuwa yakiongezeka kwa kasi.

"Serikali kupitia Wizara ya Afya, inaendelea kuwahimiza wananchi kufanya mazoezi na kupunguza ulaji wa vyakula visivyo na afya ili kuepuka magonjwa yasiyo ya kuambukiza," alisema.




Kwa upande wake, Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Temeke, Dk. Joseph Kimaro, alisema hospitali hiyo imefanikiwa kufikia upatikanaji wa dawa muhimu kwa asilimia 98 ndani ya kipindi cha mwaka mmoja na nusu.

Aidha, alisema hospitali imeajiri watumishi 120 wa mkataba katika kada mbalimbali za afya ili kuboresha huduma, hususan za kibingwa na bingwa bobezi.

Dk. Kimaro aliishukuru Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA) kwa kuchangia kiasi cha zaidi ya Sh. milioni 200 kwa ajili ya ukarabati mkubwa wa jengo la wodi ya usafishaji damu.

Aidha, uzinduzi huo umehusisha pia gari jipya la kubeba wagonjwa, ambalo litakuwa maalum kwa ajili ya mama na mtoto.

# Dk. Mpango: EAC itumie vema idadi kubwa ya vijana

**Na Mwandishi Wetu, Arusha**

MAKAMU wa Rais Dk. Philip Mpango, amesema Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), inaweza kutumia vema idadi kubwa ya watu iliyonayo hususan vijana katika kujiletea maendeleo kama itawekeza zaidi katika elimu na afya ya watoto.

Alitoa wito huo wakati akifungua Mkutano wa Elimu wa Kikanda wa EAC na Sherehe za Mwaka wa Elimu wa Umoja wa Afrika katika Ukumbi wa Mikutano wa Kimataifa wa Arusha (AICC).

Alisema ongezeko la watu katika mataifa ya Afrika Mashariki, linatoa ishara ya ulazima wa kuongeza rasilimali zaidi za kifedha ili kukidhi mahitaji ya elimu bora na afya bora.

Makamu wa Rais alisema mwenendo wa idadi ya watu Afrika Mashariki, unaweza kuwa baraka kubwa kwa kuendelea kuwa na vijana na watu mahiri wa kujenga uchumi ikiwa rasilimali watu hiyo itatumika kikamilifu.

Pia alisema kutokana na takwimu za Benki ya Dunia, Bara la Afrika limekuwa likipata matokeo ya faida katika elimu ukilinganisha na mabara mengine, lakini bado ukanda wa Kusini mwa Jangwa la Sahara, elimu imekuwa na ufadhili mdogo zaidi.

Alitoa wito wa hatua zaidi kuchukuliwa na kutumia juhudi zote kutambua kuwa changamoto za elimu barani Afrika, zinatokana kwa kiasi kikubwa na uwekezaji mdogo katika sekta hiyo, jambo ambalo linafanya kuwa vigumu kutoa elimu bora yenye ujuzi unaohitajika ili kukabiliana na maendeleo makuu matatu, ambayo ni ongezeko la idadi ya watu, utandawazi na maendeleo ya teknolojia.

Alisema Tanzania imeendelea kuchukua hatua mbalimbali katika kufanya mageuzi makubwa katika sekta ya elimu ambapo imelenga kufanya elimu ya lazima kutoka miaka saba iliyopo sasa hadi miaka 10 ifikapo mwaka 2027/28.

Aidha, alisema mabadiliko ya mtaala wa elimu nchini, yanalenga kuongeza ubora wa elimu pamoja na kuandaa rasilimali watu itakayoendana na mahitajio ya dunia ya sasa kama vile maendeleo ya dijitali, teknolojia pamoja na kutumia vema fursa mbalimbali zilizopo.

Alitaja pia hatua za uboreshaji wa miundombinu ya elimu kama vile madarasa ya kujifunzia, nyumba za walimu, kuboresha mazingira ya ufundishaji kwa kuhakikisha kuna walimu wa kutosha na nyenzo za kufundishia kama vile kompyuta na vitabu.

Alisema lengo la serikali ni kuongeza ubora wa elimu, kuongeza upatikanaji wake na kuhakikisha kuwa elimu inatosheleza katika ulimwengu wa utandawazi na maendeleo ya haraka ya teknolojia.

Aliwashukuru washirika wa kimataifa wanaoiunga mkono Tanzania katika mageuzi ya sekta ya elimu na kuukaribisha mpango mpya wa ufadhili wa Umoja wa Ulaya (PEERS) ambao utasaidia uratibu wa mifumo ya elimu katika kanda.

Aidha, alisema Tanzania ipo tayari kufanya kazi pamoja kwenye mpango kazi wa EAC katika kuendeleza malengo ya kielimu na ina dhamira ya dhati ya kuimarisha Jumuiya kwenye nyanja zote ikiwemo elimu.

Mkutano huo unahudhuriwa na viongozi mbalimbali wa AU, EAC, Mawaziri wa Elimu na wawakilishi kutoka nchi wanachama za Afrika Mashariki, wadau wa maendeleo, mashirika ya kimataifa pamoja na wadau wa sekta ya elimu.





**Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, akihutubia wakati wa Ufunguzi wa Mkutano wa Elimu wa Kikanda wa Jumuiya ya Afrika Mashariki pamoja na Sherehe za Mwaka wa Elimu wa Umoja wa Afrika uliofanyika katika Ukumbi wa Mikutano wa Kimataifa wa Arusha (AICC) jana.**

# Mwanafunzi 'anusa' kifo simu ikilipuka chumbani kwake Dar



**Mwanafunzi Albert Cosmas (mwenye fulana nyeupe), akiwa amejipumzisha nje ya chumba muda mfupi baada ya simu yake kulipuka na kusababisha moto katika chumba chao. Kushoto ni mama yake, Liana Ernest. Wengine ni wapangaji wenzake na majirani waliosaidia kuuzima moto.**



**Mwanafunzi Albert Cosmas, akimuonyesha Mwandishi wa gazeti hili chumba na mali zilizoteketezwa kwa moto baada ya simu yake ya mkononi kulipuka.**

**Na Mwandishi Wetu**

MWANAFUNZI wa Kidato cha pili katika Shule ya Sekondari Makrumula jijini Dar es Salaam, Albert Cosmas (14), amenusurika kifo baada ya simu yake ya mkononi kulipuka chumbani kwake na kusababisha moto ulioteketeza kitanda, magodoro na mali nyingine zilizokuwemo.

Tukio hilo la kutisha na kusikitisha, lilitokea katika moja ya vyumba vya nyumba ya Godfrey Kambenga, iliyoko eneo la Kimara Mwisho jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki.

Akisimulia tukio hilo, mwanafunzi huyo alisema akiwa amejipumzisha chumbani kwake majira ya mchana, alichukua simu ya mama yake, Liana Ernest, ambaye hakuwepo nyumbani na kuanza `kuchat' na rafiki yake.

Alisema wakati akiendelea na `kuchat' huku simu hiyo ikiwa kwenye soketi ikichaji, ghafla ililipuka na kuwaka moto huku ikitoa kishindo kizito.

"Nilishtuka sana na kuitupa simu chini ndani ya chumba na kukimbilia nje kujisalimisha na muda si mrefu, moto ukashika kwenye moja ya godoro na kuendelea kusambaa kwenye nguo, kitanda na vyombo vingine vilivyokuwemo ndani," alisema Albert na kuongeza:

"Nilikimbiliaa nje ya chumba na kupiga kelele kuomba msaada kutoka kwa wapangaji wenzetu aambao walikuja haraka na kuanza kuuzima moto kwa kumwaga maji chumbani hadi ulipozimika, lakini tayari ulikuwa umeshaunguza kila kilichokuwemo ndani na paa la nyumba."

Hata hivyo, alisema msamaria mwema alipiga simu Zimamoto kuomba msaada, lakini gari lao lilifika huku moto huo ukiwa tayari umezimwa na majirani kwa kutumia zana duni.

Mmiliki wa nyumba hiyo, Kambenga, alisema alifika katika chumba kilichokuwa kinaungua baada ya kusikia kelele kutoka kwa wapangaji wake.

Mama mwenye nyumba, Opportune Kambenga, alisema wakati tukio hilo likitokea, hakuwepo nyumbani na alipigiwa simu na mjukuu wake, Clara Massano na kulazimika kurejea nyumbani haraka.

" Nilikuta tayari tukio limeshatokea na nawashukuru wapangaji na majirani waliosaidia kuuzima moto na hivyo kutosambaa katika vyumba vya nyumba nyingine," alisema Mama Kambenga.

Mama wa mwanafunzi huyo, Liana alisema alitoka kidogo na kuicha simu yake nyumbani ikichajiwa na ndipo mwanawe alipoichukua na kuanza kuitumia na ndipo alipatwa na mkasa huo.

# Maoni ya Mhariri & Uchambuzi

## HII NI KERO

### Kama kuna ulanguzi wa tiketi SGR ukomeshwe

Kumekuwa na maneno ya chinichini kwamba baadhi ya wafanyakazi wa Shirika la Reli Tanzania (TRC) wasio waaminifu na madalali fulani wananunua tiketi za SGR na kisha kuwalangua watu.

Ingawa hatuna uhakika na hilo kwa asilimia 100, lakini Waswahili wanasema lisemwalo lipo, kama halipo sasa laja.

Kama ni kweli, basi hitajio la usafiri wa reli ya kisasa ni kubwa na hivyo ni wakati mwafaka, kama alivyoahidi Mkurugenzi Mkuu wa TRC, Masanja Kadogosa, kuongeza mara moja safari zaidi ili kusiwe na mtu anayekosa safari. Na kama kweli tatizo la ulanguzi wa tiketi lipo kufanyike mtego na walanguzi wakamatwe mara moja.




## MAONI YA MHARIRI

# Huduma za afya zinapoboreshwa, tuepuke visababishi

KWA sasa tatizo kubwa la kiafya la wananchi, hususani wanaoishi mijini ni magonjwa yasiyoambukiza kulinganisha na yale ya kuambukiza ambayo miaka ya nyuma ndio yalikuwa tatizo kubwa.

Magonjwa yasiyoambukiza ni pamoja na kisukari, magonjwa ya moyo, figo, matatizo ya akili, saratani, tezi dume na mengine mfano wa hayo. Kwa bahati mbaya, magonjwa haya, kama kisukari, husababaisha pia magonjwa mengine likiwemo tatizo la figo. Mbaya zaidi, tiba zake ni ghali.

Magonjwa haya yanaelezwa kwamba yanasababishwa kwa kiasi kikubwa na mtindo wetu wa maisha ukihusisha vyakula tunavyokula siku hizi vikiwemo vya mafuta mengi, kutokunywa maji ipasavyo, kukaa muda mrefu bila kwenda haja ndogo na kutofanya mazoezi.

Tunaishukuru serikali ambayo imeendelea kuboresha huduma za afya ikiwa ni pamoja na kusogeza tiba za kibingwa karibu na wananchi kila kukicha.

Kwa mfano, katika gazeti hili tuna habari ya Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kuzindua jengo la Huduma za Usafishaji Damu kwa wagonjwa wa figo katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Temeke (TRRH).

Mkuu wa Wilaya ya Temeke, Sixtus Mapunda aliyezindua jengo hilo juzi kwa niaba ya Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu anasema jengo hilo jipya la usafishaji damu ni moja ya maboresho makubwa yaliyofanyika hospitalini hapo.

Tunaipongeza serikali kwa hatua hiyo muhimu na pia tunaipongeza Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA) na wadau wengine kwa kuchangia kiasi cha zaidi ya Sh. milioni 200 kwa ajili ya ukarabati wa jengo la wodi hiyo ya usafishaji damu.

Mku wa Wilaya, Mapunda pia alitoa salamu za Waziri Ummy, akiwataka wananchi kujenga tabia ya kufanya mazoezi na kuzingatia ulaji bora wa vyakula ili kuepuka magonjwa yasiyo ya kuambukiza.

Bahati nzuri, siku hizi kupitia mitandao ya kijamii, ni rahisi ku-google na kujua visababishi vya magonjwa haya ikiwemo figo.

Ikumbukwe pia kwamba kati ya sababu 10 za vifo duniani, ugonjwa wa figo unatajwa kuwa wa saba na watalaamu wanasema moja ya sababu za kuongezeka kwa magonjwa ya figo ni pamoja na kutozingatia kupima na kuutibu katika hatua za mwanzo.

Kujua dalili pia ni suala muhimu ambapo baadhi ya hizo ni kupoteza hamu ya kula, matatizo wakati wa kulala, maumivu ya kifua, kutopumua vyema, kuvimba uso, kuumwa kichwa, kuvimba kwa miguu, kusinzia bila mpangilio, kuhisi kichefuchefu na kutapika, kukojoa damu, kukosa fahamu na hata kifafa.

La muhimu, wakati serikali inapambana kuleta tiba, ni vyema wananchi kubadilika kuhusu ulaji wetu na kupima afya zetu mara kwa mara na hasa tunapoona dalili bila kusahau kufanya mazoezi.

## Wasiliana nasi

**Mhariri Mkuu:** +255713263775 / +255748115000
**Mhariri wa Habari:** +255768411003
**Mhariri Michezo:** +255784122020
**Meneja Masoko/Biashara:** + 255718480406 / + 255733768825
**S. L. P:** 15110, Dar es Salaam
**Makao Makuu Mtaa:** Barabara ya Morogoro
**Jengo la:** Aura Mall
**Chumba Cha Habari:** +255 (0)222151532
**Email:** uelekeohabari@gmail.com

## JICHO LANGU

Hamid Yassin
0768 888 787

# Sawa Dk. Nchimbi, lakini Chadema iheshimu mamlaka

KATIBU Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. Emmanuel Nchimbi juzi alimwagiza Waziri wa Mambo ya Ndani awaachie huru viongozi wote wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) waliokuwa wanashikiliwa na Jeshi la Polisi.

Jeshi la Polisi lilianza kuwakamata Makamu Mwenyekiti wa chama hicho, Tundu Lissu, Katibu Mkuu, John Mnyika na Mwenyekiti wa Chama hicho Kanda ya Nyasa, Joseph Mbilinyi.

Naye Mwenyekiti wao, Freemani Mbowe juzi alikwenda mkoani Mbeya kwa lengo la kuwanasua wenzake mikononi mwa Polisi, lakini naye akaishia kutiwa nguvuni!

Awali, Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa nchini Tanzania iliwataka viongozi wa Chadema kusitisha kongamano la vijana lililopangwa kufanyika juzi Jumatatu, Agosti 12, 2024 katika viwanja vya Ruandazove, jijini Mbeya.

Zuio hilo lilitokana na barua iliyoandikwa Agosti 8, 2024 na Naibu Msajili wa Vyama vya Siasa, Sisty Nyahoza kwenda kwa Katibu Mkuu wa Chadema, John Mnyika ikielezea ukiukwaji wa sheria ya vyama vya siasa kutokana na kauli zilizotolewa na Twaha Mwaipaya, Katibu Mwenezi wa Bavicha.

Nakala ya barua hiyo ilitumwa pia kwa Inspekta Jenerali wa Polisi ikielezea kauli alizotoa Mwaipaya kupitia video iliyosambaa mitandaoni, ikiwahamasisha vijana kujitokeza kwa wingi pamoja na mambo mengi kwenda kuweka 'hatma' ya Tanzania juu ya masuala mbalimbali.

"Hivyo, Msajili wa Vyama vya Siasa anawaasa viongozi wa Chadema kusitisha shughuli yoyote mliyopanga kufanya siku ya Agosti 12, 2024 Mbeya au mahali popote nchini, ambayo mnajua itasababisha uvunjifu wa sheria, amani na utulivu, kwani maelezo ya Katibu Mwenezi wa Baraza la Vijana wa Chadema katika video hiyo, yanakiuka sheria ya vyama vya siasa na yanaashiria, mkusanyiko huo unaweza kutumika kuhamasisha vijana kufanya vitendo vya uvunjifu wa sheria kama ilivyotokea Kenya," ilieleza barua hiyo.

> **Hivyo, Msajili wa Vyama vya Siasa anawaasa viongozi wa Chadema kusitisha shughuli yoyote mliyopanga kufanya siku ya Agosti 12, 2024 Mbeya au mahali popote nchini, ambayo mnajua itasababisha uvunjifu wa sheria, amani na utulivu, kwani maelezo ya Katibu Mwenezi wa Baraza la Vijana wa Chadema...**

Pia, Msajili aliwataka Mwenyekiti wa Chadema, Freeman Mbowe, Katibu Mkuu wake, John Mnyika na Mwenyekiti wa Bavicha, John Pambalu kufika Ofisi ya Msajili jijini Dar es Salaam, Agosti 13, 2024 (jana) saa 5:00 kueleza kuhusu suala hilo.

Lakini kwa jeuri na kiburi viongozi wote wa Chadema walikaidi wito huo wa Msajili na kutimkia Mbeya kwenye maandalizi ya mkusanyiko huo usio na kibali wala ruksa kutoka kwenye mamlaka stahiki.

Matokeo yake viongozi wote wa chama hicho waliishia kuburuzwa 'lupango' na sasa wametoka kwa hisani ya Dk. Nchimbi, lakini wangetii amri bila shuruti yote haya yasingetokea!

Chadema iache jeuri, iheshimu mamlaka. Hata wao siku wakiwa madarakani, hawawezi kuruhusu mambo yaende kiholela hata yenye viashiria vya kuvunja amani.

# Homa ya Nyani: Kwa nini Mpox inaenea kwa kasi Afrika Mashariki na Kati?

**Na Mwandishi Wetu**

**HOMA** ya nyani, ilianza kwa wanyama kwenda kwa binadamu huko Afrika ya Kati na Magharibi, sasa inaenea kupitia wanadamu.

Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), imekumbwa na ongezeko la wagonjwa wa homa ya nyani ama Mpox. Hilo limesababisha hatua za dharura za afya kwa umma kuchukuliwa.

Uganda pia imethibitisha kesi mbili mpya za Mpox, kama ilivyo kwa Kenya, Rwanda na Burundi katika ripoti kuhusu milipuko wa homa hiyo Afrika Mashariki.

Kwa mujibu wa ripoti ya Africa CDC, idadi ya kesi zimeongezeka ikilinganishwa na mwaka jan na idadi ya vifo imeongezeka vilevile.

Umoja wa Afrika umeidhinisha Dola milioni 10.4 kutoka katika fedha zilizopo za Covid kusaidia Afrika CDC, katika kukabiliana na mlipuko wa Mpox katika bara zima.

Kesi nyingi na vifo viko DRC ambapo kwa mwaka huu pekee, kumekuwa na visa zaidi ya 8,000 vilivyoripotiwa na zaidi ya vifo 300.

Dk. Fiona Braka, Meneja wa Dharura wa Shirika la Afya Duniani nchini Congo Brazzaville, anasema "kesi zimeripotiwa katika nchi 11 za eneo hilo tangu mwanzoni mwa 2024."

"Tunaona kesi nyingi zaidi nchini DRC, ambayo inachukua asilimia 96 ya kesi zote ambazo zimeripotiwa katika eneo hili," anasema.

Visa viwili vya ugonjwa huo unaoambukiza viliripotiwa hivi karibuni nchini Rwanda na Jamhuri ya Afrika ya Kati (CAR), siku chache tu baada ya Burundi kutangaza uthibitisho wa kesi.

Hivi karibuni, nchi jirani ya Kenya pia imeripoti kisa kilichogunduliwa kwa msafiri aliyekuwa akitoka Uganda kwenda Rwanda kupitia kivuko cha mpaka kusini mwa nchi hiyo.

Hali hii imezua wasiwasi kuhusu kuenea kwa aina mpya na mbaya ya ugonjwa huo.

Afrika Kusini pia ilirekodi visa vya virusi hivyo, na vifo vitatu, lakini vipimo vya awali vinaonesha maambukizi hayo yamesababishwa na aina isiyo hatari sana ya virusi hivyo.

Wataalamu wa afya wanasema virusi hivyo vinabadilisha tabia yake, vinajitokeza miongoni mwa makundi mapya, kama vile wafanyabiashara ya ngono.

Ugonjwa huu huenea kwa njia ya mawasiliano ya kimwili na ya ngono na unaweza usigundulike kwa kutazama kwani baadhi ya watu hawaonyeshi dalili.

**MPOX NI NINI?**

Ugonjwa wa Mpox, hapo awali ulijuulikana kama monkeypox, ni ugonjwa unaosababishwa na virusi.

**Dalili zake:**

Homa, maumivu ya kichwa, maumivu ya misuli na upele unaosambaa kutoka kwenye uso hadi sehemu nyingine za mwili.

Mpox huenea kupitia mgusano wa mtu na mtu na imethibitishwa kupitia vipimo vya maabara juu ya mgusano wa vidonda vya ngozi.

Kuna aina mbili kuu za virusi vya Mpox (MPVX): MPVX Clade IIb na MPXV Clade I.

Mlipuko wa kimataifa wa mwaka 2022 ulisababishwa na aina ya MPXV Clade IIb, lakini wanasayansi wanasema aina hiyo inayoenea nchini DRC, sasa ni tofauti ya aina ya MPXV Clade I ambayo ni kali zaidi na hatari sana.


Kuna chanjo ambazo hutoa kinga dhidi ya Mpox

**Changamoto za kukabiliana nao**

Visa vya Mpox vipo zaidi katika eneo la Mashariki mwa DRC, hasa katika JIji la uchimbaji madini la Kivu Kusini-Kamituga – eneo la mpakani lenye utitiri wa wafanyabiashara, mafundi, wachimba madini na wafanyabiashara wengine.

Dk. Steeven Bilemo Kitwanda, ambaye amekuwa akifanya kazi katika kituo maalumu cha matibabu cha Mpox huko Kamituga, anasema ana wasiwasi na mienendo ya watu katika mkoa huo.

"Ni ngono zembe ndiyo inayosababisha ugonjwa huo kuenea na watu wanaokuja hapa Kamituga, hawadhibitiwi.

Wanaondoka kwenda Goma, Gisenyi nchini Rwanda, Bujumbura na kwengineko," anasema.

Kamituga ni kitovu cha kibiashara na maisha yaliyochangamka ya usiku, kumejaa baa na wafanyabiashara ya ngono.

Kwa mujibu wa Dk. Kitwanda, kesi za kwanza zilirekodiwa miongoni mwa wachimba migodi na kusababisha baadhi ya wanajamii kuamini kuwa ugonjwa huo ni laana ya Mungu kwa sababu ya uasherati.

Miongoni mwa wakazi wa eneo hilo, Mpox huonekana kuwa ni ugonjwa wa watu wasio na adabu au wahuni na unaochukuliwa kuwa ni ugonjwa wa aibu.

>>>Inaendelea Uk. 8


Kituo cha matibabu cha Mpox huko Kamituga, DRC, hutoa huduma ya haraka kwa wagonjwa na kuunga mkono juhudi za utafiti na ufuatiliaji.

# Homa ya Nyani: Kwa nini Mpox inaenea kwa kasi Afrika Mashariki na Kati?




**Dk. Kitwanda amekabiliana na milipuko kwa zaidi ya miaka 10 na alisaidia kuzuia mlipuko wa Ebola katika eneo hilo miaka iliyopita.**

>>>Inatoka Uk. 7

Dk. Kitwanda anasema unyanyapaa huu unazuia watu kutafuta usaidizi wa matibabu na umeongeza usiri kuhusu maambukizi, jambo ambalo hufanya ufuatiliaji wa watu kuwa mgumu.

Hilo huvifanya virusi kuenea bila utambuzi, haswa kati ya wanaume wanaofanya ngono na wanaume wenzao na wafanyabiashara ya ngono.

Anasema kuna haja ya kufanyika ufuatiliaji maalumu kwani mara nyingi watu huficha utambulisho wa wapenzi wao.

Watu wengi walioathirika na ugonjwa huo pia wana VVU, jambo ambalo linaweza kufanya maambukizi kuwa mabaya zaidi.

Nje ya vituo vya mijini, viongozi wanajitahidi kufuatilia virusi hivyo katika maeneo ya vijijini huku kukiwa na migogoro inayoendelea.

### Nini kifanyike?

Hatua za kimsingi za afya ya umma zichukuliwe kama vile mawasiliano, upimaji, matibabu, ufuatiliaji wa watu wanaokutana nao a ushirikishwaji wa jamii yote hayo ni muhimu ili kupambana na Mpox.

Leandre Murhula Masirika, Mátibu wa Utafiti wa Mpox nchini DRC, anasema mipaka isiyo na uangalizi ni moja ya changamoto kuu katika kukabiliana na ugonjwa huo.

"Hakuna udhibiti kwenye mipaka. Kamituga ina mipaka miwili na watu hutoka hapa kwenda Rwanda na Burundi," anasema.

Virusi hukaa takribani siku nne hadi 20 kuonekana na wakati mwingine vidonda vinaonekana tu kwenye sehemu ya siri.

Masirika anasema, hilo hufanya kuwa vigumu kugundua ugonjwa, hivyo kupima mpakani ni muhimu.

Mratibu wa utafiti anasema kuwe na mawasiliano na makundi yaliyo katika hatari kubwa ya kupata ugonjwa na unyanyapaa, ili kuzuia kuenea.

Hali nchini DRC sasa iko katika kiwango cha maambukizi ya jamii, huku wajawazito na watoto chini ya miaka mitano, wakiwa hatarini zaidi.

"Virusi hivi vimeibuka katika familia zenye watoto, mama zao na hata wajawazito, jambo ambalo limesababisha utoaji wa mimba kuongezeka," anasema Masirika.

Nchini DRC, watoto wengi, wakiwemo wachanga, wameambukizwa.

Pia kumekuwa na visa vichache vya wajawazito kuharibu mimba. Wagonjwa wengine wameteseka kwa muda mrefu na maambukizi ya macho, ngozi na sehemu za siri.

### Wito wa haraka wa chanjo

Virusi hivyo vinapoenea, wataalamu wa afya duniani, wanatoa wito wa kampeni ya chanjo.

Wakati DRC na Afrika Kusini zimeanza mchakato wa kuomba chanjo, bado hakuna chanjo iliyofika.

Marekani na Japan, zimeahidi kutoa chanjo, lakini bado hazijapelekwa.

"Chanjo haipo na watu wanakufa," anasema Masirika, Mtafiti wa Mpox.

Mapema mwaka huu, DRC ilitangaza mipango ya kutumia aina mbili za chanjo ya Mpox.

Mamlaka ya Kitaifa ya Udhibiti imeanza kukagua chanjo hizi, lakini bado hazijatolewa kwa matumizi.

Dk. Braka wa Shirika la Afya Duniani (WHO), anasema shirika lake linazidisha juhudi katika nchi mbalimbali ili kuimarisha ufuatiliaji na kuboresha mifumo ya upashanaji habari.

BBC.

# Wanaodhalilisha walimu 'walimwa' kadi ya njano

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mohamed Mchengerwa, amesema Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, hataki kusikia walimu wanapata changamoto yoyote.

"Wenye kero ngumu ngumu wasaidiwe, sijui uhamisho kwa aliyekidhi vigezo, shughulikieni, waliofukuzwa washaurini taratibu za kufuata na msijiweke mbali na watumishi," alisema.

Alisema hayo jijini Dodoma wakati akikabidhi magari kwa Makatibu Wasaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu katika mji wa Serikali Mtumba juzi.

Alisema Rais Dk. Samia anatamani kuona kila mtumishi ndani ya Tamisemi, anafurahi na kutabasamu.

"Nendeni mkatibu kero za walimu, nendeni mkamalize changamoto za walimu," alisema na kuongeza:

"Mimi mwenyewe kama Waziri mwenye dhamana, nataka nione walimu wana furaha wakati wote, nataka nione walimu wakifurahia serikali yao wakati wote.

"Nawataka wakurugenzi wasaidizi, makatibu wasaidizi wa Tume ninaowakabidhi magari leo, nendeni mkafuatilie yanayoendelea kwenye maeneo yenu" alisema.

Alipiga marufuku vitendo vya udhalilishaji dhidi ya walimu kuanzia sasa, anataka kuona wakiwa na furaha.

Alisema anatoa ujumbe huo kwa walimu kote nchini.

"Katika kipindi changu hiki, sitegemei kuona mwalimu akinyanyaswa, akionewa kwa sababu ambazo mtendaji katika eneo hilo anafanya yeye mwenyewe makusudi," alisema.

Aidha, aliielekeza Tume kuwa karibu na walimu na kuwasikiliza na kutatua kero zao.

"Tume kazi yake ni kukaa na walimu na katika kipindi changu, sitegemei kusikia mwalimu anapata msongo wa mawazo, msisubiri mimi nipigiwe simu," alisema.



**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mohamed Mchengerwa.**

Alisema kwa sasa Tume haina visingizio kwani imeshapata Bodi.

Alisema amekuwa akipokea kero nyingi za walimu na kuitaka Tume kujitahidi kuzifanyia kazi kwa haraka.

Kadhalika, alisisitiza uwajibikaji na kutambua majukumu ya kiutendaji kwa watendaji katika maeneo yao ya kazi.

# Watumia fursa ya mavuno kuchangia chakula shuleni

**Na Mwandishi Wetu, Mufindi**

WAZAZI wa wanafunzi wa shule katika Wilaya ya Mufindi mkoani Iringa, wametumia fursa ya kipindi cha mavuno kuchangia na kupeleka chakula mashuleni.

Mkuu wa Wilaya ya Mufindi, Dk. Linda Salekwa, alisema hayo juzi katika kikao cha mapitio ya Mkataba wa Lishe ngazi ya Kata, Mitaa na Vijiji katika kipindi cha robo ya nne ya 2023/24.

Dk. Salekwa alisema takwimu zinaonesha kuwa baadhi ya kata zipo chini ya asilimia 60, hali inayoonesha kuwa kuna wanafunzi hawapati chakula shuleni.

"Maofisa, nashauri mhakikishe kuwa wananchi wanatumia fursa hii ya kipindi cha mavuno, kupeleka chakula shuleni," alisema.

Kwa upande wake, Ofisa Lishe wa Halmashauri ya Mji Mafinga, Salum Atlas, alisema mashindano ya siku za vijiji lengo lake ni kuhamasisha masuala ya lishe ya kijiji na kuepukana na udumavu kwa jamii.

Naye Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Mafinga, Fedelica Myovella, alisema halmashauri hiyo imejipanga kuwatambua wanaofanya vizuri kwenye kata zao na kuonesha mafanikio na matokeo chanya.

Alisema halmashauri hiyo inatarajia kuandaa mashindano ya siku za vijiji lengo likiwa ni kuhamasisha masuala ya lishe kwa wajawazito na wanaonyesha.

*Leo ndiyo, kesho yetu*

Uelekeo

JARIDA

# Jungu kuu

Jumatano Agosti 14 - 20, 2024

UTALII
AFYA
JAMII

Jarida hili haliuzwi

UK. 12 & 13



# Zima zote washa kijani inavyopukutisha wapinzani

# Mawimbi Chadema yanapomfika Tundu Lissu shingoni



**Na Hamid Yassin**

BAADA ya Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) Kanda ya Ziwa Victoria, Ezekia Wenje kutangaza nia ya kuwania nafasi ya Umakamu Mwenyekiti Taifa wa chama hicho, joto la uchaguzi limepanda ghafla na kumchefua anayeshikilia wadhifa huo, Tundu Lissu.

Wenje ambaye kwa nafasi yake hiyo inamfanya aongoze mikoa ya Mwanza, Kagera na Geita, ameweka wazi kwamba, anakusudia kujitosa kuomba ridhaa ya nafasi hiyo inayoshikiliwa na Lissu ili amsadie kazi kwa ukaribu Mwenyekiti wake, Freeman Mbowe ambaye pengine anaamini ataendelea kuwa mwenyekiti na nafasi hiyo ya uwenyekiti wa chama hicho ambayo imeshakuwa kama ya kifalme!

Mbunge huyo wa zamani wa Nyamagama, Mkoa wa Mwanza alisema hayo Agosti 5, 2024 alipozungumza na waandishi wa habari juu ya kusudio lake hilo, akisisitiza kwamba ameamua kuwania nafasi hiyo ili kuongeza ufanisi wa kazi na uwajibikaji.

Wenje amesema baada ya tafakuri ya muda ameona ana uwezo wa kuwa msaidizi wa karibu wa Mwenyekiti wa chama hicho, Mbowe ambaye duru za kisiasa zinaonyesha atagombea tena uenyekiti kwenye uchaguzi unaotarajiwa kufanyika baadaye mwaka huu.

"Kutokana na uzoefu nilionao kwenye chama, nimejitathimini kuwa nina uwezo wa kuwa msaidizi wa Mbowe, naomba ifahamike chama chetu cha Chadema kimekuwa kikijipambanua siku hadi siku katika kupigania haki za watu, ikiwemo uhuru, haki na maendeleo," alisema Wenje.

**KUMEKUCHA**

Kwa jicho la kawaida unaweza kuuchukulia uamuzi huu wa Wenje kama demokrasia ndani ya chama kinachojiita cha demokrasia. La hasha! Utakuwa umekosea sana.

**MKAKATI ENDELEVU**

Kama una D mbili tu, utagundua kwamba huu ni mkakati endelevu wa kuipukutisha 'Timu Lissu' ndani ya Chadema.

Baada ya wafuasi wa Lissu ndani ya chama hiki akina Peter Msigwa kushughulikiwa katika chaguzi zilizopita za kanda na ngazi ya nyingine za chini, sasa umefika wakati wa kuking'oa kigogo kilichobaki.

Mbowe hajatanganza rasmi nia ya kutetea nafasi yake ya Uenyekiti wa Chadema katika uchaguzi utakaofanyika baadaye mwaka huu, lakini tayari Wenje ameshamkabidhi ushindi kabla ya uchaguzi!

Mwanasiasa huyu anaposema anataka kugombea umakamu mwenyekiti wa Chadema ili afanye kazi karibu na Mbowe, anajuaje kama bosi wake atagombea; Je, akigombea atashinda uchaguzi huo?

Hizi kauli si za kupuuzwa, hii ni mipango mkakati ya kumfukuza 'mwendawazimu na makopo yake' ndani ya Chadema. Na si mwingine bali ni Tundu Lissu anayemnyima usingizi bwana mkubwa, Mbowe!

**LISSU ASHTUKA**

Haikunishangaza pale Lissu alipoibuka katikati ya wiki iliyopita na kutoa kauli kali kwamba, Chadema si mama yake na anaweza kuondoka akiona mambo yanakwenda ndivyo sivyo!

Lissu amesema kwamba kama Baba wa Taifa hili, Mwalimu Julius Nyerere ambaye huko nyuma alikuwa akimpiga vijembe mara kwa mara, aliwahi kusema CCM si Mama yake, yeye ni nani ang'ang'anie Chadema?

"Mwalimu Nyerere katika mojawapo ya kauli zake nyingi aliwahi kusema kwamba CCM siyo mama yangu, CCM siyo mama yangu na ikiacha misingi yake nitaiacha, ilikuwa kauli ya Mwalimu kuhusu chama alichokianzisha, kwa hiyo unataka mimi niseme kwa mazingira yoyote yale, vyovyote itakavyokuwa sitahama Chadema? Ni Mama yangu?" Alihoji Lissu.

Aliongeza: "Niliingia Chadema miaka 20 iliyopita na nimekuwa hapa miaka yote hii na Mungu anirehemu niendelee kuwa hapa wakati nayo ikiendelea kuishi, lakini Chadema siyo dini na siyo mama yangu, ni chama cha siasa kikiondoka kwenye misingi yake iliyonipelekea nikajiunga nacho nitaondoka.

"Nitakuwa sina sababu ya kubaki na hiyo siyo dhambi kwa sababu hiyo siyo dini na siyo mama yangu nikitumia maneno ya Mwalimu, ni chama cha siasa, vyama vya siasa huja na kuondoka, sisi binadamu tunakuja na kuondoka," alipasua Lissu akizungumza katika Mtandao wa Kijamii wa 'Clubhouse' wiki iliyopita.

Lissu aliendelea kuanika mambo hadharani kwa kupasua kuwa, kuna tatizo la rushwa ya uchaguzi ndani ya Chadema, na yeyote anayesema hakuna tatizo hilo anawadanganya, na kusisitiza tatizo la rushwa ya uchaguzi na rushwa lipo kwenye chama chao na kupasha kuwa, rushwa ya uchaguzi dhidi ya mtu yeyote yule ni adui wa demokrasia na haki.

"Kiongozi yeyote anayepatikana kwa kununua wapiga kura, huwauza siku ikifika; kwa hiyo nilichokisema Iringa ninakisimamia kama nilivyokisema. Kuna tatizo la rushwa linatuvuruga Chadema," amepasua Lissu na kusisitiza.

"Tuangalie sisi wapigakura tuwe macho na wagombea wanaokuja kwa sababu wamenunua kugombea kwao, kwa sababu wamehonga ili wateuliwe wagombea, kwa sababu wamechafua ili waje wapate nafasi za kugombea na kuchaguliwa. Ninasimamia katika kile nilichokisema Iringa na tuwe macho."

Haya maneno yanatoka kwa kiongozi mwandamizi wa Chadema ambaye ni miongoni mwa wapinzani wachache wa kweli hapa nchini, hivyo si ya kupuuzwa hata kidogo.

**MSIGWA ALISHAWEKA HADHARANI**

Maneno kama haya pia yamekuwa yakisemwa na Mchungaji Peter Msigwa ambaye amekihama chama hicho huku akilalamikia hicho hicho anachokisema Lissu. Msigwa ambaye anaaminika kwamba alikuwa Timu Lissu na Mwenyekiti wa Kanda ya Nyasa (mikoa ya Nyanda za Juu Kusini) amekuwa akilalamika kwamba uchaguzi wa kanda hiyo ambayo Joseph Mbilinyi Sugu ambaye ni Timu Mbowe alishinda kwa rushwa.

Tumekuwa tukipiga kelele sana kwa kuandika jinsi chama hiki kikuu cha upinzani kinavyoendesha 'kisela' siasa zake za ndani ya chama na hata nje kwa kufuata kauli na amri za mtu mmoja na tunaonekana tunatumika, lakini sasa wanaibuka wenyewe na kuweka hadharani kila kitu!

*Inaendelea uk. 18*



# Mpango wa kutokomeza kunguru ulikwama wapi?

**Na Hamisi Kibari**

MIAKA ya nyuma kidogo, nchi yetu ilianzisha mkakati maalumu wa kuua ndege aina ya kunguru weusi, hususani katika jiji la Dar es Salaam. Wahusika walikuwa wamejenga mitego mithili ya vizimba, ambamo ndege hao walikuwa wakiingia na kushindwa kutoka. Nakumbuka kizimba kimoja wapo kilikuwa kwenye Viwanja vya Mwembeyanga, Temeke na maeneo mengine kadha wa kadha ya jiji la Dar es Salaam. Kwa macho yangu niliona kama ulikuwa mkakati mzuri kwa sababu kila mara nikipita pale Mwembeyanga niliona kunguru kadhaa wakiwa wamenaswa na mtego huo.

Bila shaka mpango huo ulianzishwa kwa ajili ya kutokomeza kunguru kutokana na madhara yao kama makala haya yatakavyojadili. Miongoni mwa madhara ya kunguru ni kueneza taka, kueneza magonjwa hususani kwa mifugo kama kuku pamoja na kushambulia vifaranga wa kuku majumbani. Lakini kunguru wamekuwa pia wakishambulia na kumaliza wanyama wengine wadogowadogo, wanamaliza aina nyingine za ndege wa asili na pia 'wanaiba' hata vyakula majumbami na hivyo kuogopesha watu kuanika vyakula vyao nje.

Kunguru wanaleta usumbufu mbalimbali ikiwemo watu kuogopa kubarizi chini ya vivuli vya miti ambako wanaweza kuchafuliwa na vinyesi vyao au hata vinyesi kudondokea kwenye chakula kama wanapata msosi wakiwa chini ya mti! Miongoni mwa ndege wajanja na wenye akili ni pamoja na kunguru ambao wanaweza kubeba andazi lako ukiwa hapohapo baada ya kujisahau kidogo tu. Ni ndege wabishi wasioogopa!

## KENYA WAMENZA KUWAUA

Sasa hivi, kwa mtazamo wangu, kunguru katika jiji la Dar es Salaam, bila shaka na Zanzibar wameongezeka sana na sambamba na madhara yake. Wakati tunaonekana hatuna mkakati tena wa kumaliza kunguru kama si kuwapunguza, majirani zetu wa Kenya wameanza mpango maalumu wa kupambana na ndege hao, kwa mujibu wa makala iliyoandikwa hivi karibuni na Shirika la Habari la Uingereza (BBC). Makala hiyo inasema Wakenya wameanza na awamu ya kwanza yenye lengo la kuangamiza kunguru milioni moja.

Mpango wao ni kuwaua ndege hao kwa sumu wakianza na miji ya Watamu na Malindi iliyoko katika Mwambao wa Kenya, kisha Mombasa na maeneo mengine. Kampeni hiyo kabambe ya kutumia sumu kumaliza kunguru inalenga kuhakikisha ndege hao ambao wanasonga kutoka meneo ya Pwani ya Kenya kwenda bara, hawafiki katika jiji la Nairobi.

## WALIKOTOKA KUNGURU WEUSI

Kunguru weusi, si asili ya eneo hili la Afrika Mashariki ambalo kunguru wake wa asili wana mabaka meupe na inasemekana ni kama wametoweka kutokana na kuuliwa na kunguru hawa weusi ambao ni 'wa kuja.' Inaelezwa kwamba kunguru ambao kule Kenya wanaitwa pia jina "kurabu", asili yao ni India na sehemu nyingine za Asia. Je, walifikaje Afrika Mashariki?

Zipo nadharia mbili; ya kwanza inaonesha kwamba walifika Pwani ya Afrika Mashariki kwa kudandia na kisha kusafiri na meli za kibiashara kutoka Bara Asia. Lakini nadharia ya pili na mbayo ndio inaaminika zaidi ni kwamba kunguru hawa waliletwa katika Pwani ya Afrika Mashariki miaka ya 1890, ikiwa ni jitihada za kukabiliana na tatizo la taka lililokuwa likiongezeka katika visiwa vya Zanzibar, ambavyo wakati huo vilikuwa chini ya ulinzi wa Uingereza.

Waliowaleta kunguru waliamini kwamba ndege hao watakuwa suluhisho la kumaliza tatizo la taka. Kwamba wakiingia kwenye jaa la taka, basi watakula vitu vingi hususani mabaki ya vyakula. Lakini kumbe uhalisia ni kinyume chake kwani kunguru wamekuwa ndio wasambazaji wakubwa wa taka na wakati mwingine kusambaza pia magonjwa hasa kwa mifugo kama kuku na hata kwa wanadamu.

Kutoka Zanzibar, kunguru walianza kuenea maeno ya pwani ikiwemo jiji la Dar es Salaa na pwani Kenya. Zamani kulikuwa hata na msemo wa kunguru wa Bara na kunguru wa Zanzibar, lakini kunguru wa bara sasa ni nadra kuwaona katika maeneo ya Pwani! Inaelezwa kwamba kunguru weusi walianza kuonekana kwa mara ya kwanza katika Bandari ya Mombasa mwaka wa 1947 na tangu wakati huo, idadi yao imeongezeka sana ikichangiwa na kuongezeka kwa idadi ya watu na takataka ambazo hutoa mazingira bora kwa ndege hao kula na kuzaliana.

Na mbaya zaidi wataalamu wanasema kunguru hawa weusi wanatamba wanavyoweza kwani zaidi ya binadamu hawana kiumbe hatarishi kwao ili kupunguza idadi yao kwa kuliwa na kiumbe hicho (natural predator).

*Inaendelea uk. 18*

# Zima zote washa kijani inavyopukutisha wapinzani

**Na Hamid Yassin**

CHAMA cha Mapinduzi, CCM, ni kama kimeshashinda Uchaguzi wa Serikali za Mitaa unaotarajiwa kufanyika Novemba mwaka huu na ule Uchaguzi Mkuu wa Taifa utakaofanyika mwakani, kabla ya wakati kufika!

Hii inatokana kasi mithili ya moto nyikani unaofanywa na watendaji wake wote kuanzia ngazi ya chini hadi juu hivi sasa kote nchini.

Hakuna anayekaa ofisini, kuanzia viongozi wa CCM ngazi ya taifa, wilaya, mikoa na Jumuiya zake za Wanawake (UWT) na ile ya Vijana (UVCCM), wote wako kiguu na njia kukipambania chama chao.

Mwenyekiti wa CCM, Rais Dk. Samia Suluhu Hassan amekuwa jemadari mwongoza njia, kwa kuzunguka mikoa mbalimbali kwa njia ya barabara na kuongea na wananchi sambamba na kusikiliza kero zao.

Dk. Samia amekuwa kinara wa kaulimbiu ya CCM inayotishia uhai wa vyama vya upinzani hivi sasa ya 'Zima zote, washa kijani'!

Katika ziara zake hizo, Dk. Samia amekuwa akiwahimiza wananchi kuchagua viongozi wanaopenda maendeleo kwa kaulimbiu ya; "Chagua viongozi bora wa Serikali za Mitaa kwa maendeleo endelevu ya kilimo, mifugo na uvuvi."

**VIJANA KUWEZESHWA ZAIDI**

Naye Makamu Mwenyekiti wa CCM (Zanzibar), Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi hayuko nyuma, kwani Agosti 10 alizindua kampeni ya 'Kijana na kijani' katika Uwanja wa New Amani Complex Zanzibar.

Katika hotuba yake ya uzinduzi, Dk. Mwinyi aliwahakikishia Vijana kuwa Serikali imekusudia kutenga fungu la fedha ili kuwawezesha katika elimu, ajira na uwezeshaji.

Aidha, Rais Dk. Mwinyi alieleza kuwa katika kuwainua vijana, serikali imeweka mkazo katika maeneo matatu ambayo ni pamoja na ongezeko la ajira, fungu la mikopo kuwafikia vijana na nafasi za uteuzi za uongozi.

Pia Dk. Mwinyi aliwahimiza vijana kujipanga na kujitokeza kwa wingi kugombea nafasi za uongozi katika vyombo vya maamuzi na kwamba serikali itawaunga mkono.

Rais Mwinyi pia alitumia fursa hiyo kuvishauri vyama upinzani kujifunza kwa UVCCM namna bora ya kufanya siasa na kuupongeza Umoja wa Vijana kwa kazi nzuri.

**MAMIA WATIMKIA CCM Z'BAR**

Katika hatua nyingine Dk. Mwinyi pia aliwapokea wanachama 368 kutoka vyama vya ACT Wazalendo na CUF waliojiunga na CCM wakiongozwa na Ahmed Omar aliyewahi kuwa Msaidizi wa marehemu Maalim Seif Shariff Hamad na Juma Duni Haji.

Siku moja nyuma, yaani Agosti 9, Mwenyekiti huyo wa Baraza la Mapinduzi, alikutana na makundi ya hamasa ya CCM katika ukumbi wa CCM Kisiwandui, Mjini Magharibi na kuwaambia kwamba utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi kwa asilimia 100 unalenga kukipatia ushindi wa kihistoria chama hicho katika Uchaguzi Mkuu 2025.

Dk. Mwinyi ametanabahisha kuwa, mafanikio makubwa yaliyopo katika sekta mbalimbali zikiwemo za elimu, afya, uwekezaji, mawasiliano, uwezeshaji na miundombinu, yanatokana na utekelezaji wa Ilani yao ya uchaguzi, hivyo ameyataka makundi hayo ya hamasa kueleza mafanikio hayo kwa wananchi.

Eneo jingine aliloliwekea mkazo ni kwa wanachama wa CCM kujipanga tayari kwa uchaguzi mkuu ujao pamoja na kuwahamasisha wananchi kujiandikisha na kuipigia kura CCM wakati utakapofika.

Akizungumzia uwezeshaji kwa wananchi, Makamu Mwenyekiti wa CCM (Zanzibar), Dk. Mwinyi, amewahakikishia wananchi kuwa Serikali imedhamiria kuwafikia wananchi wote ambao bado hawajapata fursa za uwezeshaji.

Dk. Mwinyi amewahimiza wana CCM kujitokeza kwa wingi kujiandikisha katika Daftari la Kudumu la Wapigakura litakapoanza mapema mwezi Januari mwakani.

**'TIMU NCHIMBI' KAZINI**

Wakati Dk. Mwinyi akiuwasha moto kule Zanzibar, huku Bara Katibu Mkuu wa Chama hicho, Dk. Emmanuel Nchimbi akiwa sambamba na Katibu wa Itikadi, Uenezi na Mafunzo, Amos Makalla na wajumbe wengine sekreterieti ya CCM wanazidi kuvipukutisha vyama vya upinzani kwa kukomba wanachama wao katika ziara zao za mkoa mmoja baada ya mwingine wanazofanya.

Kwa mfano, katika ziara viongozi hao waliyoifanya Lindi Julai 30, 2024, waliibomoa vibaya na kung'oa ngome za wapinzani mkoani humo baada ya kupokea takribani wanachama 280 wakiwemo viongozi wa upinzani ngazi za juu.

Miongoni mwa viongozi hao wajuu waliohama katika vyama vyao siku hiyo ni aliyekuwa Mwenyekiti wa ACT Wazalendo Mkoa wa Lindi na aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Mchinga mwaka 2015, Hamidu Bobali, Mwenyekiti wa Wanawake ACT Wazalendo Lindi





Mjini, Hawa Kipara na Mwenyekiti wa Chadema, Jimbo la Mchinga, Issa Sapanga.

Pia katika kundi la waliotimkia CCM alikuwemo Katibu wa ACT Wazalendo Mkoa wa Pwani ambaye alikuja kumsindikiza aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Mchinga pamoja na madiwani mbalimbali na wanachama wa vyama hivyo kujiunga na CCM.

Akizungumzia hatua yake ya kujiunga na CCM, Bobali alisema siku hiyo alikuwa anahitimisha miaka 20 ya kuwa nje ya chama cha CCM ambapo katika kipindi cha miaka hiyo, wapinzani waliweza kumwamini na kumpatia nafasi mbalimbali za kuongoza.

### KAZI NZURI YA RAIS SAMIA

Anasema kikubwa kilichomvutia ni utendaji kazi wa Rais Samia Suluhu Hassan kwa kufanya vitu mbalimbali vya maendeleo.

"Rais Samia amefanya vitu kwa macho vinaonekana wala haihitaji mtu kuniita kunishawishi bali nimeona kwa macho maendeleo anayoyafanya ikiwemo fedha za mazao ya korosho ambayo leo wakulima wote wa korosho tunapewa pembejeo bure.

"Nakumbuka mwaka 2018 niliondolewa ndani ya Bunge na kubebwa na Jeshi la Polisi nikipambana kuhusu fedha za mazao ya korosho. Leo wakulima wote tunapewa pembejeo bure bila kutoa shilingi kumi," anasema.

Pia anasema kingine kilichomshawishi kuhamia CCM ni pamoja na bandari ya Uvuvi ambayo imeanza kujengwa wilayani Kilwa mkoani Lindi ambapo serikali ilikuwa inapoteza mapato mengi kutokana na kukosekana kwa bandari hiyo.

"Leo Rais Samia ameingia ameanza kujenga bandari hiyo ambayo ina thamani ya Shilingi bilioni 266… Hili ni jambo kubwa sana kwetu," anasema.

Kwa upande wake, aliyekuwa Mwenyekiti wa Chadema Jimbo la Mchinga, Sapanga naye anasema amehama na viongozi wenzake kwenda CCM akiwemo Mwenyekiti wa Wanawake wa Chadema mkoa wa Lindi, kutokana na kazi nzuri inayofanywa na Serikali ya CCM.

"Hapa Lindi mpinzani mwenye fujo nilikuwa mimi, sasa nimehamia CCM, hapa Lindi sasa hakuna upinzani. Ninakwenda kufanya kazi na viongozi wa CCM katika kuwaletea wananchi maendeleo," anasema Sapanga.

Kule Mchinga mkaoni Mtwara, CCM iliwapokea madiwani kadhaa wa CUF na ACT na mamia ya wanachama wao walioamua kujiunga Chama hicho tawala.

Balozi Dk. Nchimbi Julai 31, 2024, akiwa mgeni rasmi kwenye Mkutano Mkuu wa Jimbo la Mchinga, kwa ajili ya kupokea taarifa ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya 2020 - 2025, kutoka kwa Mbunge wa Jimbo hilo, Mama Salma Rashid Kikwete, alipokea mamia ya wanachama wa vyama vya upinzani, wakiongozwa na hao waliokuwa madiwani pekee wa vyama vya CUF na ACT jimboni hapo.

Balozi Nchimbi pia aliwapokea mamia ya wanachama na viongozi hao, akiwemo Hussein Kimbyoko aliyekuwa Diwani wa Kata ya Milola (CUF) na Athumani Maije aliyekuwa Diwani wa Kata ya Rutamba (ACT).

Hiyo ilikuwa ni siku moja tu baada ya kuwapokea viongozi waandamizi wa vyama hivyo, pamoja na Chadema katika Mkoa wa Lindi, waliohama wakiwa na mamia ya wanachama wa vyama hivyo vya upinzani na kujiunga CCM.

Kule Kigoma nako Balozi Nchimbi mbali ya kuwahakikisha wakazi wa mkoa huo kwamba watapata umeme wa gridi ya taifa ifikapo Machi 2025, lakini pia alikomba mamia ya wanachama wapya, wakiongozwa na Diwani wa Chadema Kigoma Mjini na Diwani wa chama cha DP.

Balozi Dk. Nchimbi alisema kuwa, ahadi ya kuufungua Mkoa wa Kigoma kuwa lango kuu la biashara inaendelea kutekelezwa kwa vitendo na kusisitiza ahadi hiyo ya Rais Dk. Samia, inatekelezwa kwa hatua thabiti, kupitia miradi mbalimbali ya maendeleo ambayo inalenga kuzidi kuufungua mkoa huo, kuendelea kuunganisha na mikoa mingine lakini pia kuiunganisha Tanzania kibiashara na nchi zingine kupitia Kigoma.

### CCM YAMKARIBISHA LISSU

Mbali ya kuwanyakua wanachama na makada wa ngazi ya kati na wale wa chini, CCM pia kwa mara nyingine imemkaribisha chamani Makamu Mwenyekiti wa Chadema, Tundu Lissu.

Akiongea kwenye mkutano wa hadhara kule wilayani Misenyi mkoani Kagera, Makalla alitumia fursa hiyo kumkaribisha Lissu kujiunga na CCM akidai tayari chama chake kimeacha misingi yake.

Ukaribisho huo ulitolewa zikiwa zimepita siku chache baada ya Lissu kunukuliwa akisema Chadema si mama yake na kwamba, atakuwa tayari kukihama chama hicho endapo kitakiuka misingi iliyomfanya akaamua kujiunga nacho.

Hata hivyo, Lissu baada ya kusikia kauli hiyo ya Makalla alijibu kuwa; "Mimi nijiunge na chama chao? Yaani niende CCM kwa sababu gani au wana misingi ipi? CCM kuna nini niende kufuata? Tukajenge Taifa kwa… muulizeni Makalla anafikiria mimi nitajiunga na CCM?"

Lakini Makalla anafafanua kwamba, amemkaribisha Lissu kujiunga na CCM kwa sababu chama chake cha Chadema kimepoteza misingi yake, hivyo anakaribishwa kujiunga na CCM ili wafanye kazi pamoja kulijenga Taifa.

Makala anadai kwamba kwa sasa Chadema ni chama kisichofuata misingi ya demokrasia, kinakabiliwa na rushwa, viongozi wake hawana mpango wa kutoka madarakani na hakihubiri umoja wa kitaifa, hivyo Lissu hana sababu ya kuendelea kuwa huko.

"Kwa usomi wake Tundu Lissu, sehemu pekee ya kufanya siasa ni kwenye Chama Cha Mapinduzi. Kwa hiyo nimkaribishe ndugu yangu aje tufanye kazi, tuijenge nchi yetu," amesema Makalla.

### CHADEMA NI ADUI WA DEMOKRASIA

Aliyekuwa mjumbe wa Kamati kuu ya Chama Cha Demokrasia na Maendeleo Chadema na mbunge wa Jimbo la Iringa, Mchungaji Peter Msigwa, amewataka wananchi kutokiunga mkono chama hicho akisema kuwa ni chama ambacho hakina demokrasia ndani yake.

Mchungaji Msigwa amekuwa akisisitiza kwamba, Chadema haipambani tena na ufisadi na haisimamii tena haki na demokrasia.

Msigwa ambaye ameambatana na Katibu mkuu wa CCM Taifa, Balozi Dk. Nchimbi kwenye ziara yake mkoani Kagera anayasema hayo kwenye mikutano wa hadhara ukiwemo uliofanyika Kyaka wilayani Missenyi ambapo anaeleza kuwa adui namba moja wa demokrasia kati taifa hili ni Chadema na viongozi wake.

Kama ilivyo kwa Makalla, pia Mchungaji Msigwa anatumia jukwaa hilo kumtaka Lissu kuachana na Chadema kwa kusema kuwa imepoteza misingi yake ambayo iliwafanya kukipenda na kukiishi huku akimsihi mwenyekiti wa chama hicho, Freeman Mbowe kung'atuka maana amepoteza sifa na mvuto kwa wananchi.

Msigwa anawasihi Wanakagera na Watanzania kwa ujumla kuendelea kumuunga mkono Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kwa kusema kuwa, ndiye kiongozi mwenye nia thabiti ya kuwatumikia Watanzania huku akieleza mabadiliko aliyoyafanya kwa kipindi cha miaka mitatu ya utawala wake.

### ITAKUWAJE?

Hata nusu ya mikoa ya Tanzania viongozi wa CCM bado hawajaifikia, lakini tayari imeshaviumiza vibaya vyama karibu vyote vikubwa vya kambi ya upinzani nchini. Je, sekreterieti ya CCM ikimaliza ziara zake nchi nzima itakuwaje?

Ndiyo maana nasema kuwa, CCM imeshashinda chaguzi zijazo kabla ya filimbi kupulizwa! Wakati wao wanajijenga kwa wananchi na kuwahimiza wajiandikishe kwenye Daftari la Kudumu la Kupiga kura, huku kwingine viongozi wao wanashikana 'uchawi' kila kukicha!

Lengo la CCM kuzima 'taa' za rangi zote na kuwasha ile ya kijani pekee inakwenda kutimia asubuhi tu na mapema. Tunachosubiri ni malalamiko na madai ya Tume Huru ya uchaguzi na Katiba Mpya toka kwa wapinzani baada ya kushindwa chaguzi hizo!

*Kwa maoni na ushauri; 0768 888 787 ama 0784 122020.*



# Chatanda: Wazazi waacheni watoto wa kike wasome

**Mwenyekiti wa Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT) Taifa ambao ni moja ya Jumuiya za Chama Cha Mapinduzi (CCM), Mary Pius Chatanda amezungumzia tatizo la ndoa za utotoni kwa watoto wa kike zinazofanya wakatishe masomo yao na hivyo pia kukatisha ndoto zao na kuona kwamba ni sawa na janga baya katika jamii yetu. Akifanya mahojiano na MWANDISHI WETU, Bosi huyo wa UWT anasema tatizo la ndoa za utotoni linahitaji juhudi za pamoja za kukabiliana nalo kwani linazorotesha juhudi na kazi kubwa zinazofanywa na serikali kwa kushirikiana na wadau wengine wa maendeleo katika kuinua elimu nchini.**

UELEKEO: Hongera Mheshumniwa Mwenyekiti kwa kuaminiwa na wana-CCM wanawake kuendesha jumuiya hiyo. Kwa ufupi sana unaweza kueleza maendeleo ya UWT chini ya uongozi wako?

CHATANDA: Ahsante sana. Wanawake wameniamini kwa sababu wameona ninao uwezo wa kushirikiana nao katika kujiletea maendeleo yahusuyo wanawake, watoto na wananchi kwa ujumla. Aidha, wanawake wameona nina uwezo wa kuhamasisha kushiriki shughuli mbalimbali za kijamii, kiuchumi na kisiasa. Kwa hakika, UWT inaendelea vizuri na tunashiriki kikamilifu katika shughuli za ujenzi wa chama na maendeleo ya nchi kwa ujumla.

UELEKEO: Tunazo sekta nyingi za huduma za kijamii na moja ya sekta hiyo ni elimu. Unaweza kutuambia kwa nini Chama Cha Mapinduzi na serikali yake vimeipa msukumo mkubwa sekta ya elimu katika ngazi zote za elimu?

CHATANDA: Chama Cha Mapinduzi kimeipa msukumo mkubwa sekta ya elimu kwa sababu elimu ndiyo ufunguo wa maisha na maendeleo kwa ujumla. Kwa kuwa CCM kimedhamiria kuwaletea wananchi wake maendeleo, hivyo ajenda ya kuinua elimu ni ya kudumu na hatuwezi kujitenga nayo kwa kuwa ni nyenzo ya kufanikisha maendeleo ya wananchi.

Ndiyo maana Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais wetu mpendwa na Mwenyekiti wa CCM, Dk. Samia Suluhu Hassan imewekeza fedha nyingi kuboresha elimu kuanzia elimu ya msingi, sekondari hadi vyuo vikuu. Serikali inatoa elimu bila malipo hadi kidato cha sita na pia kwa elimu ya juu vijana wanapata mikopo ambayo sasa imeshuka hadi ngazi ya diploma.

Kwa kifupi, CCM ni elimu na elimu ni CCM. Si rahisi kupata maendeleo ya haraka bila kuwekeza kwenye elimu. Tutapata wapi watalaamu wa kuendesha nchi hii kama hatujawaandaa kupitia mfumo wa elimu? Tutapata wapi hata viongozi wanaokwenda sambamba na mabadiliko ya sayansi ya teknolojia bila kuwekeza vya kutosha kwenye elimu?

UELEKEO: Umekuwa kinara wa kupigania elimu ya mtoto wa kike. Tueleze kinachokupa msukumo mkubwa katika eneo hilo?

CHATANDA: Nimekuwa kinara kupigania elimu ya mtoto wa kike kwa sababu bado katika jamii yetu (hata karne hii) zipo imani potofu kwa baadhi ya watu kuwa mtoto wa kike hana umuhimu wa kwenda shule. Wanaamini mtoto wa kike ni wa kusaidia kazi za nyumbani na kusubiri kuolewa, basi. Wanaofanya hivyo hawajali kwamba watoto wote ni sawa, awe wa kiume au wa kike kwani wote wanastahili kupata elimu na wote wanaweza kufanya kazi yoyote zikiwemo zile za kitalaamu.

Lakini tukumbuke misemo ya wahenga kwamba ukimwelimisha mtoto wa kike umeelimisha jamii nzima (lakini unapoelimisha mtoto wa kiume unaelimisha mtu mmoja tu). Hivyo mtoto wa kike anapopata elimu tunakuwa tumeelimisha jamii nzima na kuharakisha maendeleo ya familia, jamii na nchi kwa ujumla. Kuna msemo wa Kiarabu unasema mama ni shule. Kwa hiyo tunahitaji kuwa na mama wengi ambao wamesoma pia.

UELEKEO: Bado kuna tatizo katika nchi yetu la watoto wa kike kukatisha masomo yao na kuolewa. Wapo hata wazazi ambao huwahimiza watoto wao wa kike wajifelishe makusudi ili iwe sababu ya kutoendelea na masomo ili kuolewa na kuepuka mkondo wa sheria, unadhani ni nini kinasababisha kuendelea kwa ndoa za utotoni (hata katika karne hii) na nini wito wako katika kutokomeza tatizo hili?

CHATANDA: Ni kweli, kuna baadhi ya watoto wa kike wamekatishwa masomo na kuolewa na hii ni kutokana na baadhi ya wazazi na walezi kuendelea na mtazamo wa mfumo dume na kuamini mtoto wa kike hastahili kuendelea na masomo bali kuolewa. Lakini wako baadhi wanataka kupata mahari kama kitega uchumi jambo ambalo pia si sawa (kumfanya mtoto wa kike kitegema uchumi kupitia mahari). Wito wangu kwa wazazi na walezi wenzangu tuone umuhimu wa kuwapeleka watoto shule bila kuwabagua ili kuwasaidia katika maisha yao ya sasa na ya baadaye na ili wawe sehemu ya maendeleo ya nchi yao.

UELEKEO: Inaonekana baadhi ya wazazi na walezi wanaamua kuozesha watoto wao wa kike kwa kutojua madhara ya kufanya hivyo. Nini madhara ya ndoa za utotoni?

CHATANDA: Kimsingi, madhara ya ndoa za utotoni yapo mengi, mathalani, watoto wa kike kukosa haki ya kuendelea na elimu, wengine wanapata maradhi ya kuambukiza kama vile Ukimwi na kupata msongo wa mawazo (stress).

Lakini pia wanashindwa kuhimili ndoa hizo kwani uwezo wao wa kufikiri na kupambana na pilikapilika za ndoa pamoja na ulezi wa watoto huwa bado mdogo. Lakini pia yapo matukio ya watoto hawa kupata matatizo wakati wa kujifungua kutokana na kupata ujauzito wakati via vyao vya uzazi vikiwa havijakomaa.

UELEKEO: Ni kwa namna gani, kwa ujumla wake, ndoa za utotoni zinazorotesha juhudi za maendeleo ya nchi yetu?

CHATANDA: Serikali inawekeza fedha nyingi kwenye utoaji wa elimu, kwa hiyo watoto wa kike wanapoolewa na kuacha masomo ni hasara kwa serikali ambapo fedha hizo zingeweza kutumika kwenye kutoa huduma nyingine za kijamii kama maji, afya umeme na kadhalika.

Lakini pia, kama nilivyokwishaeleza, ndoa hizi zinakatisha ndoto za hawa watoto. Pengine miongoni mwao wangekuwa madaktari, walimu, wanasiasa wakubwa na kadhalika lakini wanabaki kuwa mama wa nyumbani zaidi. Hata kilimo, biashara na ufugaji siku hizi pia vinahitaji elimu ili kwenda na kilimo au ufugaji wa kisasa na kutafuta masoko.

Pia ndoa za utotoni sambamba na mimba za utotoni, zinazorotesha maendeleo kwa sababu wapo wengine uwezo wa kufanya kazi unapungua kutokana na wengine kutelekezwa baada ya kupata ujauzito hata hawaelewi wafanye nini ili waweze kujikimu kimaisha. Na hivyo watoto wanakuja bila maandalizi na kuwa mzigo kwa jamii na hata wazazi. Na hii inaweza pia kuwa sababu ya watoto kupata udumavu kwa mama huyu mtoto kukosa lishe bora akiwa mjamzito na hata baada ya mtoto kuzaliwa kukosa lishe.

Vilevile ndoa za utotoni zinaongeza talaka katika jamii kwani watoto wa kike wanakuwa hawajakomaa vizuri kuhimili changamoto za kifamilia na hivyo badala ya jamii kujikita kufanya shughuli za maendeleo, kazi inakuwa kwenye kusuluhisha migogoro ya kifamilia.

UELEKEO: Una wito gani kwa wazazi na serikali katika mapambano ya ndoa za utotoni?

CHATANDA: Niwashauri wazazi na walezi wabadilike, wawe mstari wa mbele kupinga ndoa za utotoni. Wasiwe sehemu ya kuunga mkono watoto wao kukatisha masomo bali wasimame kidete kupinga na kuhakikisha ndoto za watoto wao wa kike zinatimia. Wazazi na walezi wenzangu chondechonde msiozeshe watoto wangali wadogo. Tuwaache wakue wapate elimu na ubongo wao utakuwa umekomaa na kuweza kutambua zuri na baya na namna anavyoweza kujitegemea mwenyewe.

Aidha, ni vyema wazazi wawe wanatenga muda wa kuzungumza na watoto wao na si vibaya kurejea mila na desturi nzuri za kuwafundisha watoto wetu maadili ya Mtanzania. Nirudie tena kusema wazazi msiozeshe watoto wenu wa kike, waacheni wasome. Kwa upande wa serikali, ni kuendelea kutoa elimu ili wananchi watambue madhara ya ndoa za utotoni na kuwachukulia hatua kali za kisheria wale wote wanaokatisha masomo ya watoto wa kike.

UELEKEO: Nikushukuru sana Mwenyekiti wa UWT Taifa kwa ushirikiano wako.

CHATANDA: Ahsante sana, karibu tena. Wanawake ni jeshi kubwa tupo imara katika kusaidia mapambano ya mimba na ndoa za utotoni. Pia, tupo imara kushiriki katika shughuli za maendeleo kwa kuhakikisha wanawake wanakuwa sehemu ya kufanikisha juhudi za maendeleo kuanzia ngazi ya familia, jamii na nchi kwa pamoja.



Mary Pius Chatanda

# Zijue mbinu rahisi za kutengeneza pembejeo za asili, mavuno kibao

**Na Mwandishi Wetu**

MWANZONI mwa Mwezi huu nchi yetu iliadhimisha takribani siku 10 za sherehe za wakulima, maarufu Nanenane katika kanda mbalimbali mchini huku kitaifa sherehe hizo zikifanyika katika Kanda ya Kati, kituo kikiwa Viwanja vya Nanenane Nzuguni, jijini Dodoma.

Maonesho ya Nanenane yamekuwa na umuhimu mkubwa kwa wakulima na wafugaji kutokana na kutoa nafasi katika eneo moja ambalo wakulima hupata wasaa wa kujifunza mbinu mbalimbali za kilimo na ufugaji wa kisasa.

Hivyo kutembelea maonesho ya Nanenane kwa mkulima ni jambo muhimu sana kama atataka kujua mengi yenye tija kwa wakati mfupi.

Ingawa kilele cha Nanenane kilikuwa Agosti 8, na kuendelea kwa siku mbili kwa maana ya Agosti 10, mpango wa sasa ni kufanya viwanja vya maonesho hayo kutofungwa mara baada ya siku hizo, bali mabanda na bustani zilizoko kwenye eneo la maonesho kuendelea kutoa huduma kwa mwaka mzima hadi maonesho mengine ya mwaka ujao.

Kwa mfano, Mkurugenzi Msaidizi wa Masoko, Wizara ya Kilimo, Happy Kitingati anasema kwambva katika viwanja vya Nanenane kutakuwa na vivutio mbalimbali ili wakulima na wafugaji waendelea kuvitembelea kwa mwaka mzima.

"Tunataka Viwanja vya Nanenane Dodoma, kwa mfano, kuwe na kila aina ya vivutio kama vile hoteli. Litakuwa eneo la viwanda vitakavyochakata mazao ya kilimo katika kusaidia kukuza pato la taifa na kufanya viwanja hivi kutumika mwaka mzima. Mtu akienda akute kuna shughuli inaendela pale," anasema.

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule yeye anasema kutakuwa na sehemu ya kulaza wakulima katika viwanja hivyo.

"Pamoja na juhudi za kuendeleza kilimo (katika) eneo la Maonesho ya Nanenane Dodoma (ambalo halitafungwa kusubiri Nanenane nyingine), kutakuwa na eneo la kulaza wakulima wanaotaka kujifunza. Watapata fursa ya kupewa elimu, maarifa na ushauri wa masuala ya kilimo kupitia wataalamu watakaopatikana kwenye viwanja hivyo muda wote," anaema Senyamule, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma

### KILIMO IKOLOJIA HAI

Katika maonesho ya Nanenane mwaka huu kulikuwa na mengi ya kujifunza ikiwa ni pamoja hili ambalo makala haya yanaliangazia kwa kina. Hili ni wakulima kutakiwa kutumia mashirika yanayohamasisha kilimo ikolojia hai, ili kujifunza mbinu za kutengeneza viuatilifu na mbolea kwa njia ya asili.

Ushauri huo unatolewa na wataalamu wa kilimo ikolojia hai kutoka Shirika la Kilimo Endelevu Tanzania (SAT) na Kilimanjaro Permaculture Community (KPC), wakati walipozungumza na mwandishi wa makala haya.

### GHARAMA NAFUU

Daudi Gwabara, Meneja Miradi Msaidizi kutoka SAT anasema kutengeneza viuatilifu na mbolea asili hauna gharama na ni salama kwa mkulima, ardhi na mazingira.

Anasema Tanzania ni moja ya nchi yenye rasilimali asili nyingi ambazo zikitumika vizuri kwenye kilimo, asilimia 100 ya mazao yatakuwa yamezalishwa kwa mfumo wa kilimo ikolojia hai ambao u akubalika duniani kote.

Gwabara anasema Shirika la SAT ambalo lipo mkoani Morogoro limewezesha zaidi ya wakulima 3,000 nchini kutumia mbinu za kilimo ikolojia hai na matokeo yake yamekuwa makubwa katika ubora wa mazao na soko la uhakika.

Anasema rasilimali za kilimo ikolojia hai zinapatikana shambani, hivyo ni rahisi kwa mkulima yoyote kuzitumia na kwea gharama ndogo.

### VITU VINAVYOTAKIWA KUUA WADUDU

Gwabara anasema mchakato wa kutengeneza viautilifu vya asili unahitaji, molasesi lita mja, tangawazi kilo moja, kitunguu saumu kilo mbili, pilipili kali kilo mbili, konyagi chupa kubwa au pombe kali lita moja na vinega lita moja.

"Tunaposema dawa ya kudhibiti wadudu waharibifu ipo shambani ni katika muktadha huu, kwamba mkulima anaweza kununua molasesi lita moja, tangawizi kilo moja, kitunguu saumu kilo mbili, pilipili kali kilo mbili, konyagi kubwa na vinega lita moja vitu ambavyo mkulima yoyote anaweza kununua kwani gharama haizidi shilingi 50,000," anasema.

Mtaalamu huyo anasema baada ya kuchanganya vitu hivyo na kupata lita 16 hadi 20 mkulima anatakiwa kuchukua lita tatu hadi tano na kuchanganya na lita 100 ya maji ambapo ataweza kupulizia shamba lenye hekari 20 na kuendelea.

Gwabara anasema mchanganyiko huo ukikamilika unatambulika kama kiuatilifu kinachoitwa Apichi, hivyo kuwataka wakulima kutumia teknolojia hiyo ambayo ni rahisi.

"Inasikitisha sana mkulima anatumia gharama nyingi kununua dawa za viwandani, huku gharama ya kupuliza shamba la ekari 20 anaweza kutumia Apichi iliyogharimu shilingi 50,000 au chini ya hapo. Lazima tubadilike, tupende vitu vya asili kwa teknolojia hii inalinda afya ya mkulima, mlaji, udongo na mazingira," anasema.

Mtaalamu huyo an asema matumizi ya teknolojia ya asili kwenye kilimo inachangia chakula kuwa na ladha nzuri, virutubisho na kuhakikishia usalama wa afya kwa watumiaji.

Gwabara anasema mchakato mzima wa kutengeneza kiuatilifu cha Apichi unahitaji siku tano, ili mkulima aweze kutumia na mimea kuwa salama.

### KUTENGENEZA MBOLEA YA ASILI

Akizungumzia mchakato wa utengenezaji wa mbolea ya asili, Gwabara anasema wanatengeneza kwa kutumia bidhaa ambazo ni rahisi pia kupatikana.

"Tunatengeneza mbolea yenye kirutubisho cha nitrojeni, tunatumia bidhaa zinazopatikana kwa mkulima kama matunda ya nanasi, papai lilokomaa na kuiva, molasesi na maziwa ambayo yametoka kukamuliwa kwa kuwa yana vitamini nyingi, kwani bakteria wanaoenda kuchachusha wanapata chakula," alisema.

Anasema molasesi inatumika kama nyenzo ya kuongeza nguvu kwa bakteria kukuwa na kuzaliana kwa wingi.

Mtaalamu huyo anasema mbolea hiyo inavunda baada ya kukaa siku 30 ambapo mkulima anaweza kutumia kuotoesha na kukuzia mazao.

Gwabara anasema lita tatu hadi tano ya mbolea hiyo inapaswa kuchanganywa kwenye lita 100 ya maji ambapo matumizi ni kila mmea kupata mbolea kiasi cha robo lita.

"Iwapo mkulima analima kilimo cha kitalu anaweza kuunganisha katika mfumo wa umwagiliaji wa dripu na kuweza kusambaza shamba nzima na mimea ikaweza kupata mbolea safi na salama," alisema.

Anasema mazao kama mpunga








mkulima anaweza kutumia njia ya solo ambayo inaweza kusambaza kwa urahisi kwenye mimea yote ya jamii hiyo.

Mtaalamu huyo anasema pia wanatengeza mbolea ya kukuzia mimea ambayo inaitwa Super Magro ainayotengenezwa kwa kutumia kinyesi, molasesi, maziwa na majivu ambayo yanasaidia kupunguza PH.

Anasema mbolea hiyo baada ya kutengenezwa inakaa siku 30 ndipo ianze kutumika kwa kuweka kila shina robo lita na mazao yataweza kukuwa kwa haraka bila shida yoyote.

Gwabara anasema teknolojia hiyo imepokelewa na wakulima katika Wilaya za Kongwa, Morogoro, Chamwino, Mpwapwa, Dodoma, Simanjiro, Masasi, Karatu, Kigamboni, Mbaralim, Kilosa na baadhi ya wilaya za Mkoa wa Njombe na kwingine.

Anasema wadudu ambao ni viumbe hai wana manufaa katika kilimo, hivyo wanapaswa kukabiliwa na njia za asili ili kuhakikisha hawadhuriki.

"Ni katika muktadha huo sisi watu wa kilimo ikolojia hai tunasema dawa ya kukabiliana na wadudu wasumbufu au mazao kutokua kwa haraka ipo shambani na sio viwandani kama ambayo inahamasishwa kwa sasa," anasema.

Anasema utafiti ambao wamefanya kwenye mashamba ambayo yalikuwa yakitumika kwa kilimo cha mbolea na viautilifu vya viwandani, baada ya kubalidilika na kutumia mfumo wa kilimo ikolojia hai mavuno yameongezeka mara dufu, huku ardhi ikiwa safi na salama.

### MBOLEA ZAIDI ZA ASILI

Kwa upande wake Mkurugenzi wa KPC, Frank Marwa anasema katika kilimo ikolojia hai wanatambua mbolea za aina tatu ambazo ni mbolea ya kupandia, kukuzia na ya kunenepeshea mazao kama matunda.

"Mbolea ya kupandia tunatumia majaji ya kijani na kijivu, udongo wa porini wenye bakteria nyingi, mbolea ya mifugo ambapo mchanganyiko wake ukifanyika vizuri inatumika katika kilimo. Mbolea ya mboji ipo ya siku 14, 30, miezi mitatu, sita hadi mwaka," anasema.

Marwa anasema pia wanatengeza mbolea asili inayotokana na mabaki ya gesi ya kinyesi cha ng'ombe.

Anasema mbolea hii baada ya gesi kuzalishwa, kipo kinyesi ambacho kinabaki, hivyo kikichakatwa kwa kufuata utaratibu na kupunguza ukali uliopo ili isiungeze mazao.

"Ipo mbolea inayokana na mabaki ya chakula kama karoti, nyanya, kitunguu na vinginevyo, ambayo inaandaliwa kwa kuweka kwenye chombo cha taka kama dumu ambalo unalitoboa na kuweka nyasi kavu na minyoo wekundu wanaozosha mbolea baada ya kuweka takataka.

Minyoo watakuwa wanameng'enya mabaki ya chakula, hivyo maji yakayotoka ndio yanafaa kwa mbolea," anasema.

Marwa anasema mbolea hiyo inatumika mahususi kwa ajili ya kukuzia na kunenepesha matunda kwa kuwa ina kiwango kukubwa cha potashiamu manganise, nitrojeni na kalishamu.

Anasema wanashauri wakulima kutumia mbolea hizo kwa kuwa zina uwezo mkubwa wa kukuza mazao, kutunza ardhi kwani ardhi hii tumeazimwa, mazingira na afya ya mlaji.

Pia Marwa anasema wametengeza teknolojia nyingine ya kuchuja maji taka na kutumika kwa ajili ya umwagiliaji, hivyo kuwataka wakulima wawatumie ili kupata elimu hiyo.

"Nyumbani kwetu tunazalisha maji taka, hivyo tumekuja na teknolojia ambayo inatumia ndoo na kuweka mawe na majaji ambayo yanachuja maji hayo na kuweza kumwagilia nyumbani bila gharama kubwa. Na mfumo huu unaweza kutumika katika mazingira ambayo hayana maji ya kutosha," anasema.

Naye Mkulima, Abdi Kiduka kutoka Wilaya ya Chemba anasema teknolojia hiyo ambayo inatumia rasilimali zinazopatikana shambani inapaswa kuungwa mkono ili kuhakikisha wakulima wazalishaji mazao bora na salama kwa mlaji.

Kiduka anasema serikali inahitajika kushirikishiana na wadau wa kilimo ikolojia hai kuhakikisha kundi kubwa la wakulima linafikiwa kwa haraka, ili kuweza kutengeneza kizazi bora.

Mkulima wa Kilimo Ikolojia Hai kutoka MVIWAMORO, Tatu Magongo anasema mbinu ya kuandaa kiuatilifu kisicho na kemikali kwa njia asili inapaswa kufikia wakulima wengi.

Magongo anasema amekuwa akilima kwa nia za kilimo ikolojia hai kwa muda mrefu hivyo ni wakati wa kuendeleza taaluma hiyo kwa wakulima wenzake.



## Kurunzi

Na Dk. Reubeni Lumbagala | 0620 800 462

# Zima zote washa kijani, mtaji muhimu wa CCM

Imekuwa ni kawaida pale ambapo wizara, taasisi, shirika au chama cha siasa kinapokuwa na jambo lake linalohitaji uungwaji mkono kutoka kwa wananchi na wadau wengine huja na kampeni maalumu yenye ujumbe wa hamasa ili kufanikisha kutimia kwa lengo hilo.

Mathalani, Wizara ya Afya katika kuhakikisha wananchi wanatunza afya zao ina kampeni yake ya "Mtu ni afya, jali afya yako", Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) kwa upande wake katika kukabiliana na rushwa ya ngono kwenye vyuo vikuu ikaja na kampeni ya "Vunja ukimya kataa rushwa ya ngono."Hii ni mifano michache ya kampeni zilizoendeshwa hapa nchini katika kuhakikisha elimu inawafikia umma kikamilifu ili malengo yaliyokusudiwa yaweze kufanikiwa.

Chama Cha Mapinduzi (CCM) ambacho uwepo wake madarakani unatokana na uungwaji mkono kutoka kwa wanachama wake, wananchi na wengine wasio na vyama, kimeendelea kufanya jitihada kubwa kuhakikisha kinaungwa mkono kwa wingi ili kiweze kuendelea kuongoza nchi kwa kuwatumikia wananchi katika nafasi mbalimbali za uongozi wa nchi yetu kuanzia nafasi za uongozi wa serikali za mitaa ambako ndiko wananchi wengi waliko hadi kwenye udiwani, ubunge na urais.

Hakuna ubishi kwamba, kwa kutekeleza ilani yake ya uchaguzi vyema, kila mwananchi anaona namna serikali ya CCM inavyopambana kumaliza kero za wananchi na kunyanyua uchumi wa mtu mmoja mmoja na wa nchi kwa ujumla, lakini hiyo haitoshi, ndio maana kupitia viongozi wake wabunifu wanakuja na mbinu nyingine za kuifanya CCM iendelee kuwa kwenye mioyo ya wananchi. Ni katika muktadha huo, CCM kupitia Umoja wa Vijana wa CCM (UVCCM) umezindua kampeni yake isemayo "Zima zote, washa kijani."

Kampeni hii ni mahsusi yenye kuhamasisha wanachama na wananchi kujiandikisha kwenye daftari la kudumu la wapiga kura na vijana kujitokeza kwa wingi kugombea nafasi mbalimbali za uongozi kuelekea uchaguzi wa serikali za mitaa mwishoni mwa mwaka huu na baadaye uchaguzi mkuu mwakani.

Katika chaguzi hizi, wagombea watakaopitishwa na CCM kugombea nafasi mbalimbali za uongozi watakwenda kushindana na wagombea kutoka vyama vya upinzani. Hivyo basi, CCM kupitia UVCCM umeona ni wakati mwafaka kuhakikisha kinazidi kujijenga zaidi kwa kuhakikisha kinahamasisha wanachama na wananchi kwa ujumla kujiandikisha ili kuwa na mtaji wa kura na hatimaye kuendelea kushinda kwa kishindo.

Wanachama wa CCM na wananchi waliojiandikisha kwenye daftari la kudumu la wapiga kura au kuhuisha taarifa zao na hatimaye kujitokeza kupiga kura kuchagua wagombea watokanao na CCM kunatoa uhakika wa ushindi na hatimaye CCM kubaki madarakani na kuendelea kuwatumikia wananchi.



> **Nataka vijana mlichofanya leo hapa ndio kikafanyike mikoani, wilayani, kata, vijiji hadi kwenye vitongoji jambo litakalosaidia kuleta tija na kupata ushindi tuliokusudia.**
>
> Issa Ussi Gavu

Julai 6, 2024 Katibu wa NEC Idara ya Organaizesheni na Mlezi wa jumuiya za chama hicho, Issa Ussi Gavu alimwakilisha Katibu Mkuu wa CCM Taifa, Dk. Emmanuel Nchimbi kwenye uzinduzi wa kampeni ya zima zote washa kijani iliyofanyika Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam. Halafu mwishoni mwa wiki, Agosti 10, kampeni hii ikahamia Zanzibar ambako mgeni rasmi alikuwa Makamu Mwenyekiti wa CCM (Zanzibar) ambaye pia ni Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi.

Katika uzinduzi wa kampeni hiyo, Gavu alisema; "Nataka vijana mlichofanya leo hapa ndio kikafanyike mikoani, wilayani, kata, vijiji hadi kwenye vitongoji jambo litakalosaidia kuleta tija na kupata ushindi tuliokusudia."

Mbali na kampeni kuhamasisha wananchi, hususani vijana kujiandikisha ili wapate sifa za kupiga kura, vilevile inawahimiza vijana kujitokeza kwa wingi kugombea nafasi mbalimbali za uongozi katika uchaguzi wa serikali za mitaa na uchaguzi mkuu wa mwakani ili waweze kuwa sehemu ya watoa maamuzi kwa manufaa ya nchi yao.

Ikumbukwe kuwa vijana ni nguvu kazi ya taifa ambayo ikitumika vyema, taifa litapiga hatua kubwa za kimaendeleo kwa haraka na pia vijana wana mitazamo yao ambayo inapaswa kuwa na uwakilishi sawia kwenye vyombo vya maamuzi ikiwa ni pamoja na vikao vya halmashauri na Bunge.

Halikadhalika, kwenye vyama vya siasa, vijana ni wadau muhimu kwa kuwa wana uwezo wa kujenga hoja, wanaweza kutumia muda mwingi kujenga chama kwani wana nguvu kutokana na umri wao.

Vijana wana uwezo wa kutembea kwa miguu umbali mrefu kuzunguka maeneo mbalimbali kujinadi na kunadi wagombea wengine wa chama chao wasio vijana kueleza kazi nzuri zilizofanywa na Mwenyekiti wa CCM Taifa ambaye pia ni Rais wa nchi Dk. Samia Suluhu Hassan, wabunge na madiwani ili lengo la kuungwa mkono na wananchi liweze kutimia na kufanikiwa.

Kimsingi, kama nilivyodokeza hapo juu, chama cha siasa ili kushinda chaguzi ni lazima kiwe na mtaji wa wapiga kura wa kutosha. Ushindi wa chama unaanzia kupitia ushawishi wa wanachama, wakereketwa, mashabiki na wananchi kwa ujumla kujitokeza kwa wingi kujiandikisha katika daftari la kudumu la wapiga kura, zoezi linaloendelea sasa nchini.

Ikumbukwe kwamba ni katika kundi hili la vijana, wamo wale ambao katika chaguzi zilizopita mwaka 2019 na 2020 (zaidi miaka minne mitatu iliyopita) hawakuwa wapiga kura kwa sababu walikuwa hawajafikisha umri wa miaka 18 ili waweze kutambulika kama watu wazima na kuweza kupiga kura.

Baada ya kukamilika uandikishaji wa wapiga kura na wengine kuboresha taarifa zao wakiwemo waliohama maeneo au kupoteza vitambulisho vya kupigia, vyama vinapaswa kuchagua wagombea bora wanaokubalika ndani na nje ya chama na mwisho kabisa wanachama na wananchi kwa ujumla kujitokeza kwa wingi kupiga kura kuchagu watu watakaowafaa.

Kama alivyowahi kusema Mwanamajumui, Profesa Patrick Lochi Otieno Lumumba kwamba uchaguzi ni sawa na kuwapa wananchi hundi isiyoandikwa chochote (blank cheque) ili wajaze humo 'mahela' wanayotaka na hivyo ni kipindi muhimu sana. Michakato yote hii inahitaji hamasa ya chama kwa wanachama wake na wananchi kwa ujumla ili kuhakikisha ushindi wa kishindo unapatikana kwa kuwa CCM inajinasibu kuhakikisha inaleta wagombea makini na sahihi.

Ndiyo maana UVCCM ikaja na kampeni ya zima zote washa kijani ili kuhakikisha kuwa michakato yote hii inafanikiwa na chama kinaendelea kuongoza katika ngazi zote na kuwatumikia wananchi kwa kutatua kero zao. Kampeni hiyo pia inalenga kutoa dira kwa wagombea watakaopitishwa na chama wawe ni wenye uwezo wa kuwatumikia wananchi na wasiwe wale wanaotafuta uongozi kwa rushwa.

Kutokana na umuhimu wa vijana katika kufanikisha ushindi wa chama, Gavu anasema "Niwahakikishie vijana watakaojitokeza kugombea chama hakitamwacha kijana ambaye alionekana kujitolea kwa jamii pindi jina lake litakapopelekwa kwenye kupitisha majina ya wagombea."

CCM inawahamasisha vijana wake kujitolea kwa moyo wote kukijenga chama chao na kugombea nafasi mbalimbali za uongozi badala ya kuwa wabeba mikoba ya wagombea. Ili taa ya CCM iweze kuzizima taa nyingine za vyama vya upinzani ni lazima kuwepo na umoja na mshikamano wa wanachama na kuepuka makundi na migawanyiko.

Ni vyema kampeni hii ihamasishe pia uadilifu miongoni mwa vijana na wanachama wengine na kupinga vitendo vyote vya rushwa ili mgombea apitishwe kwa uwezo wake wa kujenga hoja, kukubalika kwake na kuwa na moyo wa kuwatumikia wananchi na si fedha au mali alizonazo.

Nirudie kusisitiza kwamba suala la chama kutoa wagombea wanaokubalika ni muhimu kuzingatiwa ili kurahisisha ushindi, ndiyo maana Mbunge wa Chalinze (CCM) na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu Ridhiwani Kikwete alihimiza sana kuhakikisha CCM inapitishe wagombea wanaokubalika katika jamii.

"Hata kama kuna mwanachama wa Chama Cha Mapinduzi ambaye yeye mwenyewe wala hataki mambo hayo, jamii pale inamtaja vizuri, mfuateni na mumwambie kama wewe mwenzetu kila tukikaa kijiweni tunasema kama kuna mtu mzuri wa kutuongoza basi ni yule pale ambaye ni wewe, utatuletea mambo mazuri eneo letu. Basi mfuateni na mwambieni ili kukisaidia chama chetu lakini kutafuta wale marafiki zenu ambao mnauza nao mapori, kutafuta marafiki zenu mnaofanya nao ubadhirifu wa mali za umma, ni kukiingiza chama kwenye mtihani mkubwa sana," anasema Ridhiwani Kikwete.

Kampeni hii ikienda vyema, bila shaka itakuwa mtaji mkubwa wa CCM kushinda kwa kishindo katika chaguzi hizi ambazo ziko mbele yetu lakini pia itachangia kutupatia viongozi bora wakiwemo vijana mashababi.

Ikumbukwe kwamba katika miaka ya karibuni kumekuwa na tatizo pia la watu wengi kutojitokeza kupiga kura, sababu kubwa ikiwa watu kudharau wakisema 'Hata nisipokwenda kupiga kura atapatikana tu kiongozi... Ni kupoteza muda tu." Ni vyema kampeni hii ijikite vyema kwenye eneo hilo kwani unaposhindwa kwenda kupiga kura maana yake unaruhusu watu wengine wakuchagulie kiongozi ambaye pengine wewe hukumpenda au kiongozi mbaya. Katika hali hiyo utakuwa hauna haki ya kulalamika kama katika eneo lako mtakuwa na kiongozi wa hovyo. Tafakari, chukua hatua.

*Mwandishi ni mwalimu wa Shule ya Sekondari Mlali iliyoko wilaya ya Kongwa mkoani Dodoma.*



Paul Mng'ong'o
KLINIKI YA FIKRA
Simu: 0676055444 Email: mngongopaul@yahoo.com

WEWORK CONSULT

# Dondoo za matumizi sahihi ya muda



Matumizi sahihi ya muda ni moja ya mambo muhimu kuyazingatia ili kufikia hatma unayoikusudia. Watu wengi wamekuwa wakiimba dhana hii bila mafanikio na kujikuta wakipoteza muda mwingi kwa vitu visivyo na matunda.

Tunapoongelea matumizi sahihi ya muda ni kuhakikisha muda wako unatumika kwenye vitu ulivyopanga na vinavyokuletea matokeo.

Leo Kliniki ya Fikra inaangazia dondoo muhimu zitakazokusaidia kuutumia muda wako vizuri. Tafadhali Fuatana nami: -

**KUWA NA MPANGO WA MAMBO YAKO (PLAN)**

Watu wengi wanaishi na kufanya mambo yanayokuja tu. Ni muhimu kupanga siku zako na kuhakikisha kila muda upo kwenye mpangilio.

Ukiweza kupanga ni hatua kubwa kukufanya utumie muda wako vizuri. Andaa ratiba yako ya siku, wiki au mwezi na hata mwaka ukionesha mambo muhimu kwa wakati husika, utayafanya lini na kwa rasilimali zipi?

Hakikisha una orodha ya mambo yako ya kufanya kila siku (To do List), tumia kalenda mtandao (Kama vile google calendar), weka vitu vya kukumbusha kama vile Reminders, Alarm, nk. Dalili ya mtu kufanikiwa ni kuwa na mpango rasmi wa mambo yake.

**KUWA NA VIPAUMBELE (PRIORITIES)**

Baada ya kuwa na orodha ya mambo ya kufanya, ni muhimu kuweka vipaumbele ili kujua nini kinaanza na kipi kunafuata. Ni muhimu ukiamka tu, uwe unajua ninaanza na nini na kinachofuatia ni nini.

**ANZA MAPEMA (START EARLY)**

Hii ni siri itakayokupa hamasa ya kuutumia muda wako vizuri. Ili kulifanikisha hili; lala mapema, lala saa za kutosha zinazoshauriwa kitaalamu, na ndipo utafanikiwa kuamka mapema na kuanza ratiba zako mapema. Pia ili ufanikiwe vizuri kwenye majukumu yako, anza kwa sala (maombi), anza na mazoezi mepesi kisha anza na mambo rahisi ili kukupa hamasa.

**CHANGANUA KILA JUKUMU LAKO (BREAKDOWN EVERY TASK)**

Ukijipa jukumu la kufanya, lichanganue vizuri. Mfano, ukiweka lengo la mwaka ni kujenga nyumba, basi anza kuchanganua lengo hilo kwenye "tasks" ndogondogo kama vile, lini unatakiwa kununua kiwanja, mpaka lini utanunua matofali, unahitaji cement ngapi, nondo ngapi, mbao kiasi gani, gharama ya ufundi ipoje, bati, milango, madirisha, umeme, bomba, nk. Hapa utakuta ndani ya lengo moja kubwa, kuna kazi au malengo madogo mengi. Haya yatakupa kujua sasa uhalisia wa ugumu au wepesi wa jukumu kuu.

**GAWA MAJUKUMU (DELEGATE TASKS)**

Kama upo na watu, ni vizuri sana ukigawa majukumu. Usilazimishe kufanya kila kitu mwenyewe. Hii itakupa faida nyingi kama kukamilisha mambo kwa haraka, kurithisha uwezo, kuwapa nafasi wengine kukua, itakuongezea uzoefu wa usimamizi, nk.

**WEKA MALENGO JANJA (SMART GOALS)**

Malengo yako ili yatimie hakikisha ni malengo mahsusi (Specific), yanayopimika (Measurable), yanatekelezeka (Achievable), ni malengo halisia (Realistic) na pia yawe na muda maalum na ukomo (Time bound). Malengo yenye sifa hizi, hayatakupotezea muda kwenye kuyasimamia kutimia.

**USITOKE NJE YA MALENGO (AVOID DESTRUCTION)**

Ukishaweka malengo ni muhimu sana kuwa makini na mwangalifu ili usitoke nje ya malengo. Hii inaitwa "Focus" Usianze kuvutiwa au kutamani malengo ya watu. Mfano social media, maongezi, wageni wengi na marafiki, kupokea majukumu ya kusaidia na kutamani njia za watu.

**SEMA HAPANA KWENYE BAADHI YA MAMBO**

Ili ufanikiwe kutumia muda wako sawasawa lazima uwe na uwezo wa kusema hapana kwenye mambo ambayo hayapo kwenye ratiba zako na hususani yale ambayo hayana mchango chanya kwenye malengo yako.

**SHUGHULIKIA MSONGO WA MAWAZO (AVOID STRESS)**

Ili kutumia muda wako vizuri shughulikia mambo yanayoweza kukutia kwenye msongo wa mawazo au kama tayari upo kwenye hilo tatizo basi shughulikia kwa hekima. Msongo wa mawazo una tabia ya kumpotezea muda sana mhusika na kumwacha kwenye njiapanda kwa muda mrefu.

**EPUKA KUFANYA MENGI KWA WAKATI MMOJA (MULT-TUSKING)**

Pamoja na kuwa utafiti unaoonesha kuwa wanawake wanaweza kufanya mambo kadhaa kwa wakati mmoja, lakini ni vizuri sana ukafanya jambo moja kwa wakati mmoja. Hii itakujenga zaidi kuliko kuwa na mambo mengi kwa wakati mmoja.

**PUMZIKA**

Ukitaka kuwa na matumizi mazuri ya muda, pumziko. Pumzika katikati ya kazi ili kurudisha umakini (Time off – 5 minutes room), fanya mapumziko ya mwili na jiburudishe (Refreshments)

**FUATILIA MALENGO YAKO KUHAKIKISHA YANATIMIA KWA WAKATI NA RASILIMALI ZILIZOPANGWA**

Hii itakufanya usisubiri hadi mwisho wa kazi kugundua kuwa kazi zooote zimeharibika uanze upya. Fuatilia kwa nyuma kuhakikisha kila kitu kinaenda vyema na maeneo ya kurekebisha, fanya mapema.

**JITATHMINI (EVALUATION)**

Hili ni jambo muhimu sana kwenye kutunza muda wako kwa sababu bila kujifanyia tathmini za mara kwa mara, utajikuta unarudia makosa yaleyale mara kwa mara, jambo ambalo ni upotevu mkubwa wa muda.

Wework Consult - Your Partner in Growth

# Mawimbi ya Chadema

*Inatoka uk. 10*

Lissu maji yamemfika shingoni. Ameona ajitetee kabla hayajamfunika pua! Sasa anasema ukweli yuko tayari kufuata nyayo za akina Msigwa, kwani Chadema si mama yake!

Kufuata nyayo za Msigwa? Ndiyo, si umesikia kauli zake katika majadiliano yale ya Mtandao wa 'Clubhouse' kwamba, kauli za Msigwa juu ya Chadema zisipuuzwe!

Lussu anasema kuwa, inategemea hayo maneno mabaya anayoongea Mchungaji Msigwa dhidi ya Chadema yanahusu kitu gani na anayoyatoa ni nani, kama ni tuhuma za matumizi mabaya ya madaraka, za ubadhirifu na ufujaji wa mali za chama hata kama yametolewa na mtu aliyeondoka.

"Katika mazingira haya ya ndoa kuvunjika yanahitaji yapimwe ili kama ni ya kweli hatua zichukuliwe, na sisi sio malaika, sisi sio mitume sisi ni chama cha siasa kinachoongozwa na binadamu, inawezekana kuna makosa mahali, sasa huyu anayetoa tuhuma pamoja na kwamba anatoa tuhuma baada ya kutoka nje hizo tuhuma ama zinahusu mambo mazito kama hayo niliyoyataja zinahitaji ziangaliwe na kutolewa maelezo kwa sababu kuzinyamazia hivihivi siyo sawa," amepasha Lissu na kuongeza.

"Kama ni za kweli usipozitolea maelezo maana yake ni kwamba unaficha uovu, unaficha uchafu, na kama sio za kweli vilevile zioneshwe kwamba sio za kweli na katika hayo ambayo ameyasema Peter Msigwa nilisema yanahitaji kujibiwa kwa sababu ni masuala ambayo uthibitisho wake upo kwenye nyaraka, akaunti za chama zinasemaje, orodha ya mali za chama zisizohamishika ni ipi?" Amehoji Lissu.

Kiongozi huyo mwandamizi wa Chadema amesisitiza kuwa, licha ya tuhuma hizi kutolewa na mtu aliyewakimbia katika mazingira tatanishi kama hayo, lakini hizi tuhuma zinahitaji kujibiwa na kutolewa maelezo ili wanachama na umma waondokane na taharuki ya haya yanayosemwa.

Naam; kwa kauli hizi za Lissu naona kuanzia sasa tuanze kuhesabu siku tu kabla ya mwanasiasa huyu kubwaga manyanga pale Chadema, maana ni kama ninawaona 'Timu Mbowe' walivyofura baada ya matamko haya ya Makamu Mwenyekiti wao.

Ndiyo maana Wenje anaibuka hivi sasa na kutangaza nia ya kuitaka nafasi ya Lissu, uamuzi wake huu haukuja kama ajali, bali ni jambo ambalo ukiunganisha nukta kama wanavyosema wazungu unaona kabisa lilipangwa ili kumvuruga Tundu na wamefanikiwa, kwani tayari jamaa keshatutangazia; "Chadema si Mama yangu!"

### LISSU NA NDOTO YA URAIS

Ni mwezi uliopita tu, Julai 26, Lissu alitangaza nia ya kugombea Urais wa Tanzania kwenye Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025 kwa tiketi ya Chadema, lakini kabla hata wiki mbili hazijaisha anaibuka tena na kutuambia Chama hicho si 'Mama yake'!

Lissu aliweka wazi kuwa, nia yake ipo palepale kama alivyogombea Urais mwaka 2020 na mwakani atatia timu uwanjani!

Baada ya tangazo lake hilo, niliandika makala ya kumtahadharisha juu ya azma yake kwamba asidhanie itakuwa rahisi kihivyo kwa chama chake kubariki nia yake.

Nilimwambia kuwa, ni jambo zuri kwake kutangaza nia yake mapema kama alivyofanya ili aanze kupima upepo kutoka pande mbalimbali kama maji aliyoyavulia nguo atamudu kuyaoga!

Nikampasha ukweli kwamba, atakabiliana na upinzani mkali kutoka ndani na nje ya chama chake kutokana na maadui wengi aliowatengeneza yeye mwenyewe. Tayari sasa analia kuwa, Chadema si 'Mama yake' na anaweza kutimka chamani kwa kile alichodai atakavyoona misingi iliyomfanya akajiunge na chama hicho ikikiukwa!

Nilimwambia asidhani kuwa, kigingi cha yeye kuwania urais kitakuwa Chama Cha Mapinduzi pekee, la hasha! Atakuwa amekosea sana; nikamsisitizia kwamba, mtihani wa kwanza kwake ataupata kutoka ndani ya chama chake, Chadema.

Mimi si mpiga ramli lakini duru za kisiasa kwa kuunganisha nukta nilisema zinaonyesha Mwenyekiti wake, Freeman Mbowe naye anataka kujaribu bahati yake ya kuukwaa urais wa Tanzania, akigombea kwa mara ya pili baada ya kuanguka vibaya mwaka 2005 mbele ya Rais mstaafu Jakaya Mrisho Kikwete.

Nikasema hivi sasa Chadema kuna kambi mbili, ile ya 'Timu Mbowe' na ya 'Wafia Lissu'! Nikamuuma sikio asidhani kambi hizi zimeibuka kwa ajili ya uchaguzi wa ndani tu wa chama hicho, hapana. Hii ngoma ni hadi kumpata mgombea wao wa urais mwakani!

Mbowe keshaapa kwamba, lazima atetee nafasi yake ya uenyekiti wa Chadema na mwakani iwe isiwe, yeye ndiye atapeperusha bendera za chama hicho kwenye kugombea urais. Patamu hapo!

Nilimwambia naamini analijua hili, ndiyo maana amekuwa akimpiga vijembe bosi wake huyo katika patashika za uchaguzi wao wa ndani kwamba, amemwaga fedha chafu kuhakikisha watu wake anaowataka wanashinda kwenye chaguzi zote za ngazi ya chini zikiwemo zile muhimu za ngazi ya kanda zote za chama hicho.

Haya ndio matokeo ya aliyekuwa kiongozi muhimu wa chama hicho, Mchungaji Peter Msigwa kutimkia Chama tawala, CCM, baada ya kupigwa nyundo ya uhakika ya siasa kule kwenye uchaguzi wa Kanda ya Nyanda ya Juu na 'Timu Mbowe'!

Nilimpasha kuwa, anajua wazi kwamba hawa viongozi wanaochaguliwa kwa mlango wa uani ni kwa ajili ya kwenda kutumika kumrudisha Mbowe kwenye kiti chake cha enzi sambamba na kupitisha jina lake kuwa mgombea wao wa urais katika Uchaguzi Mkuu wa nchi hapo mwakani.

Yote niliyoandika kwenye makala ile ndiyo haya ambayo hivi sasa Lissu mwenyewe anajitokeza hadharani kuyathibitisha! Yaani maji yamemfika shingoni, anapambana yasije mfika hadi puani yakamziba pumzi!

### MPANGO WA MABADILIKO

Lakini akina Profesa Kitila Mkumbo, Zitto Kabwe na Samson Mwigamba walipoandika Waraka wa Mkakati wa Mabadiliko ndani ya Chadema baada ya kumshitukia Mbowe hadi wakafukuzwa walionekana wataka madaraka.

Wakati Dk. Wilbrod Slaa anaondoka Chadema, akina Zitto walimkumbusha kwamba kile walichokuwa wakipigania kwenye mpango huo mwaka 2013 ni ukiukwaji wa misingi ya haki na demokrasia lakini Slaa hakujali mpaka yalipomkuta!

Ninamshauri Lissu na viongozi wengine wa Chadema waudurusu tena huo waraka kwani ulianisha sura zote Mbowe na genge lake.

Baadhi tu ya sura hizo ni kwamba amegeuza chama kuwa mali yake na harusu demokrasia linapokuja suala la nafasi yake, kwamba haruhusu watu kumpinga kile anachokitaka, kwamba yeye na genge la wanaomzunguka wanakula fedha za chama kama hawana akili nzuri na kwamba hakuna mikakati yoyote ya maana ya kuimarisha uhai wa chama na kukipatia mapato zaidi ya kutegemea maandamano.

Kadri ninavyoona, Lissu una njia mbili tu; kubaki Chadema huku ukiona misingi ya haki na demokrasia ikivunjwa na kuvumilia ama kutimkia chama mbadala, maana chama si kabila kwamba huwezi kulibadili, wala siyo 'mama yako mzazi' kwamba unachelea kukosa radhi. Mimi ninakushauri kama ambavyo Katibu wa NEC ya CCM, Itikadi ya Uenezi na Mafunzo, Amos Makalla amekuwa akikushauri pamoja na Mchungaji Msigwa. Hama!

*Kwa maoni na ushauri; 0768 888 787 ama 0784 122 020.*

# Mpango wa kutokomeza kunguru

### HATARI KULIKO NDEGE WOTE

Kunguru hawa weusi kwa kwa mujibu wa makala hiyo, wanatajwa kuwa wavamizi na waharibifu zaidi ya ndege wote ulimwenguni.

"Wanawinda wanyama wa asili, sio ndege tu bali pia mamalia na wanyama watambaao - na hivyo athari zao kwa bioanuwai ni mbaya," Jaap Gijsbertsen, mtaalamu wa ndege wa Uholanzi, ambaye anazuru eneo la Watamu nchini Kenya, ameiambia BBC.

Wahifadhi wa mazingira nchini Kenya pia wamekaririwa wakisema kwamba kunguru hao wamepunguza kwa kiasi kikubwa idadi ya ndege wadogo wa asili katika ukanda huo kwa kupasua viota vyao huku wakilenga mayai na vifaranga.

"Wakati idadi ya ndege wa asili inapungua sana, mazingira yanaanza kuathirika. Kunakuwa na ongezeko la wadudu waharibifu ambao kwa kawaida huwindwa na ndege au wanyama wadogo na wataambao wa asili (lakini viumbe hao wanaliwa na kunguru)," Lennox Kirao, mwanasayansi wa utafiti katika kikundi cha uhifadhi wa mazingira cha A Rocha Kenya, anasema.

Eunice Katana, mfugaji wa kuku wa kienyeji anayeishi katika kijiji cha Takaye, kaunti ya Kilifi anasema: "Wanarukia vifaranga na kuwala kama vichaa. Hawa sio ndege wa kawaida yaani wanaweza kukupa hasara ya vifaranga ndani ya dakika chache tu." Kunguru pia wanaelezwa na wataalamu kwamba hutumia sauti yao ya kipekee kuwasiliana wanapoona hatari au wanapoona mawindo.

Kwa mujibu wa BBC, kunguru pia wamelalamikiwa kuharibu nyumba mjini Mombasa kwa kujisaidia kwenye kuta na paa. "Kunguru hawa huamka mapema na hukatiza usingizi wetu kwa milio yao ya kuudhi na kupiga kelele," anasema mkazi wa Mombasa, Victor Kimuli.

Mbali na maeneo ya kutupa taka, hoteli za kitalii zimekuwa pia kimbilio kubwa la kunguru, ambapo humiminika sehemu za kulia chakula na kuwabughudhi wageni wanapokuwa wanafurahia mlo wao, wamiliki wa hoteli wamelalamika. "Kunguru kwa kweli wamekuwa kero kubwa kwa wageni wanaotembelea hoteli zetu kufurahia milo yao nje ya ufuo wa tropiki," Maureen Awuor, Mwenyekiti wa Chama cha Wahudumu wa Hoteli na Wahudumu wa Kenya, anasema.

Baadhi ya hoteli huwatega kunguru huku nyingine zikiwakodisha vijana wenye manati ili kuwatia hofu na kuleta utulivu kwa watalii, hatua inayowaongezea gharama.

Kuhusu hatua ya kuwatega inasemekana haileti ufanisi wa kutosha kwa kuwa kunguru wana akili ya kunusa hatari na kuepuka maeneo ambayo wameshuhudia kunguru wengine wakifa au kunaswa.

### KUWAUA NI JIBU

Ni kwa kuzingatia haya, ndio maana mamlaka nchini Kenya zimeamua kuchukua hatua zinazolenga kuwaangamiza ndege hawa ambao hawana faida yoyote kwa kuwaua kwa kutumia sumu. Kenya wamechukua hatua ya sasa baada ya kuwepo kwa mashauriano na wataalamu wa mazingira, wahifadhi, viongozi wa jamii na wawakilishi kutoka sekta ya hoteli na Shirika la Huduma ya Wanyamapori nchini Kenya (KWS). "Tunajaribu kupunguza idadi yao hadi kiwango kinachoweza kudhibitiwa (kama si kuwamaliza kabisa)," anasema Kirao.

Mchakato wa kuwaua unahusisha kupata maeneo na kuwawekea chambo hususani nyama.

"Wakishazoea, kisha tunawatilia sumu baada ya kukusanyika kwa idadi kubwa zaidi katika maeneo hayo yenye chambo," Eric Kinoti, Afisa kutoka A Rocha Kenya, anasema. Anasema sumu inayoitwa Starlicide ndio hadi sasa imeonekana inafaa zaidi katika zoezi la kuwaua kunguru na kupunguza idadi yao, bila kuathiri ndege au wanyama wengine.

Takriban kunguru 2,000 waliuawa mwaka 2022 wakati wa uchunguzi wa ufanisi wa sumu hiyo uliofanywa na kampuni ya Little Kenya Gardens, iliyopewa leseni ya kuingiza sumu hiyo kutoka nje ya nchi, Cecilia Ruto, mmiliki wa kampuni hiyo, anasema.

"Sumu hii inayofanya kazi taratibu humezwa na kunguru kabla ya kufa na kuna hatari ndogo sana ya sumu hii kuua wanyama wengine ambao hula mizoga ya kunguru waliokufa," Cecilia Ruto anaongeza. Anasema sumu hiyo ambayo Kenya wanaiagiza kutoka New Zealand, kilo mbili zina uwezo wa kuua takribani kunguru 20,000.

Hata hivyo, matumizi ya sumu nchini Kenya yameibua makundi ya wanaharakati wa haki za wanyama na ndege, ambao wanahoji kuwa kuwapa kunguru sumu ni unyama na kwamba mbinu mbadala na zisizo za kuua zinapaswa kuchukuliwa.

"Kutumia sumu ni suluhisho la muda mfupi ambalo halishughulikii kiini cha tatizo," anasema Leonard Onyango ambaye ni mwanaharakati wa mazingira akimaanisha zitumike mbinu kama za kuwafanya wasizaliane au kumaliza mayai yao.

"Kuna haja ya kuangalia mbinu endelevu na za kiutu kudhibiti idadi ya kunguru," anaongeza.

Lakini wahusika katika mpango huo wa kutumia sumu unaoungwa mkono na wananchi wengi wanasisitiza uhitaji wa kulinda viumbe vya asili vinavyomalizwa na kunguru hao na kuhakikisha kunakuwa na usawa wa kiikolojia wakati wote.

"Ikiwa hatutafanya lolote sasa, uharibifu unaweza kuwa mkubwa na usioweza kurekebishwa baadaye," anasema Kirao na kuongeza kwamba kwa sasa sumu ndio jibu.

Anasema hii si mara ya kwanza kwa serikali ya Kenya kuanzisha mipango ya kudhibiti aina ya ndege vamizi. Kwamba miaka 20 iliyopita Kenya pia ilipunguza idadi ya kunguru lakini mpango haukuwa mzuri kama wa sasa wa kuchagua maeneo ya kuwawekea chambo.

### KUNGURU WAKARIBIA NAIROBI

Licha ya idadi kubwa ambayo imepangwa kuuawa, viongozi wanaona kuwa hawana chaguo, hasa kwa kuwa kuna wasiwasi kwamba kunguru wanaweza kuenea ndani ya nchi ya Kenya kama hatua hazitachukuliwa sasa.

Ndege hao wameonekana katika eneo la Mtito Andei, takriban kilomita 240 (maili 150) kutoka mji mkuu, Nairobi, wahifadhi wanasema.

"Hofu yangu kubwa ni kwamba, tusipofanya lolote sasa, kunguru watafika Nairobi. Hili litakuwa tishio kubwa kwa wanyama na ndege nchini, haswa katika Mbuga ya Taifa ya Nairobi," Kirao anasema.

### TANZANIA TUKO WAPI?

Kwa kuwa kunguru wanaendelea kuwa tishio, Watanzania tuna kila sababu ya kwenda kujifunza Kenya tukiona inafaa ili tuanze tena kuwapunguza kama si kuwamaliza kabisa kunguru katika jiji la Dar es Salaam na Zanzibar kama wao pia wanakumbana na adha tunazokumbana nazo Dar. Kama ilivyoelezwa kwamba kunguru ni wajanja kung'amua mitego mimi ninashauri Watanzania twende moja kwa moja kwenye sumu na majirani zetu wameshaturahisishia kazi ikiwa ni pamoja na kufanya majaribio ya sumu hiyo ya Starlicide.



# Matumaini kufikia makubaliano kusitisha mapigano yazidi kufifia

**KHARTOUM, Sudan**

MATARAJIO ya makubaliano ya kusitisha mapigano kutokana na mazungumzo ya amani nchini Sudan yaliyofadhiliwa na Marekani wiki hii, hayapo mezani kwa sasa, kwani pande zinazopigana hazijathibitisha kuhudhuria kwao.

"Tumekuwa na mawasiliano ya awali na RSF. Tumekuwa na mawasiliano ya kina na Jeshi la Sudan (SAF). Lakini bado hawajatupa uthibitisho ambao ungekuwa muhimu leo ili kusonga mbele Agosti 14,", Tom Perriello, Mjumbe Maalum wa Marekani kwa ajili ya Sudan, aliwambia waandishi wa habari mjini Geneva juzi Jumatatu.

Perrielo alisema: "Tutasonga mbele na washirika wetu wa kimataifa kufikia mpango wa utekelezaji, mpango wa utekelezaji madhubuti kuhusu jinsi gani tunaweza kusonga mbele hadi kukomesha ghasia na kupata usambazaji kamili wa misaada ya kibinadamu, na utaratibu wa ufuatiliaji wa utekelezaji. Mambo haya yalikuwa yafanyike muda mrefu uliopita."

Umoja wa Mataifa unauchukulia mzozo wa Sudan kama mzozo mbaya zaidi wa kibinadamu duniani. Mzozo huo mbaya ambao umeikumba Sudan umesababisha zaidi ya watu milioni 10.7 kuwa wakimbizi wa ndani ya nchi na kuwalazimisha wengine milioni mbili kukimbilia nchi jirani kutafuta hifadhi.

VOA.

# Muungano Wafanyakazi Usafiri wa Anga Kenya watishia kugoma

**NAIROBI, Kenya**

MUUNGANO wa Wafanyakazi wa Usafiri wa Anga Kenya, umesema wafanyakazi wa Shirika la Ndege la Kenya Airways na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Kenya, wataanza mgomo kuanzia Agosti 19, mwaka huu kufuatia pendekezo la uwekezaji kutoka kampuni ya India ya Adani Airport Holdings, kwenye Uwanja Mkuu wa Ndege nchini humo.

Mgomo huo huenda ukasababisha usumbufu mkubwa kwa Shirika la Ndege la Kenya Airways na kwa shughuli za Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Jomo Kenyatta jijini Nairobi, kitovu muhimu cha usafiri barani Afrika.

"Tutafikiria tena azma yetu ya kushiriki katika hatua ya viwanda, ikiwa tu mkataba wa Adani Airport Holdings Limited, unaachwa kabisa," alisema Moss Ndiema, Mkuu wa Muungano wa Wafanyakazi wa Anga Kenya.

Mwezi uliopita, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege vya Kenya ilisema kuwa pendekezo la uwekezaji kutoka Adani Airport Holdings ilijumuisha njia ya pili ya kuondokea ndege kwenye Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Jomo Kenyatta. VOA.

> **Tutafikiria tena azma yetu ya kushiriki katika hatua ya viwanda, ikiwa tu mkataba wa Adani Airport Holdings Limited, unaachwa kabisa"**




## Ukraine yadhibiti km 1,000 za mraba ndani ya Urusi



**KYIV, Ukraine**

KAMANDA Mkuu wa Ukraine, Oleksandr Syrskyi, amesema vikosi vya Kyiv vinadhibiti kilomita za mraba 1,000 za ardhi ya Urusi huku wakiendeleza uvamizi wao mkubwa wa kuvuka mpaka katika miaka miwili na nusu ya vita.

Kamanda Syrskyi alisema Ukraine iliendelea "kuendesha operesheni ya kimkakati katika eneo la Kursk" siku saba baada ya kuanza.

Rais wa Ukraine, Volodymyr Zelensky, alisema Urusi imeleta vita kwa wengine na sasa vinarejea kwao.

Lakini kiongozi wa Urusi Vladimir Putin, alielezea shambulio hilo kama "uchokozi mkubwa" na akaamuru vikosi vya Urusi kumfukuza adui nje ya eneo lao.

Idadi inayoongezeka ya watu, wamehamishwa kutoka eneo la Magharibi mwa Urusi kwa usalama wao, huku wengine 59,000 wakiamriwa kuondoka.

Gavana wa eneo hilo alisema baadhi ya vijiji 28 vimetekwa na vikosi vya Ukraine, na kwamba raia 12 wameuawa na "hali bado ni ngumu".

Wanajeshi wa Ukraine walifanya shambulizi lao la kushtukiza Jumanne iliyopita, na kusonga hadi kilomita 30 kuingia Urusi.

Mashambulizi hayo yanasemekana kuongeza ari kwa upande wa Ukraine, lakini wachambuzi wanasema mkakati huo unaleta hatari mpya kwa Ukraine.

Chanzo kikuu cha kijeshi cha Uingereza, ambacho hakikutaka jina lake litajwe, kiliiambia BBC kwamba kuna hatari Moscow itaghadhabishwa na uvamizi huo kiasi kwamba inaweza kuongeza mashambulizi yake yenyewe dhidi ya raia na miundombinu ya Ukraine.

BBC.

# FBI yachunguza madai ya kulengwa kambi ya Trump

**WASHINGTON, Marekani**

SHIRIKA la Ujasusi la Marekani (FBI) limeanzisha uchunguzi kuhusu madai kuwa kambi ya kampeni ya Trump ililengwa na wadukuzi wanaofanya kazi kwa ajili ya Serikali ya Iran.

"Tunaweza kuthibitisha kuwa FBI inachunguza suala hilo," shirika hilo lilisema katika taarifa fupi siku ya Jumatatu bila kumtaja rais wa zamani au Iran.

Msemaji wa kambi ya kampeni ya Trump aliiambia BBC kuwa hati hizo zilipatikana kinyume cha sheria na "vyanzo vya kigeni vinavyoichukia Marekani".

Hata hivyo, maafisa wa Iran wamekanusha kuhusika na udukuzi huo na Serikali ya Marekani haijaishutumu rasmi Iran.

FBI pia inachunguza ikiwa wadukuzi wa Iran walilenga kambi ya Joe Biden-Kamala Harris, kulingana na CBS News, mshirika wa habari wa BBC, akinukuu watu wanaofahamu uchunguzi huo.

Taarifa ya kambi ya kampeni ya Trump imetolewa siku moja baada ya Microsoft kutoa ripoti inayoonyesha kwamba wadukuzi wa Iran walilenga kampeni ya mgombea urais wa Marekani ambaye hakutajwa jina Juni, mwaka huu.

Mwishoni mwa wiki, Trump alisema wadukuzi waliweza tu kupata habari zilizokusudiwa kutolewa kwa umma".

Kulingana na gazeti la Washington Post, wafanyikazi watatu wa kambi ya kampeni ya Biden-Harris pia walilengwa na barua pepe za ulaghai siku chache kabla ya Rais Joe Biden, kutangaza kwamba anajiondoa kwenye kinyang'anyiro cha kuingia Ikulu.

Msemaji wa kambi ya kampeni ya Harris alisema katika taarifa yake kwa vyombo vya habari kwamba "wanafuatilia kwa uangalifu na kuhakikisha ulinzi dhidi ya vitisho vya mtandaoni na hatufahamu ukiukaji wowote wa usalama wa mifumo yetu".

BBC.




## Uingereza yaitaka isiishambulie Israel

**LONDON, Uingereza**

WAZIRI Mkuu wa Uingereza, Sir Keir Starmer, ameitaka Iran "kujizuia" kuishambulia Israel wakati wa mazungumzo ya simu na Rais mpya wa Iran.

Sir Keir alimwambia Masoud Pezeshkian kulikuwa na "hatari kubwa ya kufanya makosa na sasa ulikuwa wakati wa kutulia na kuzingatia kwa makini".

Ni mazungumzo ya kwanza kati ya Waziri Mkuu wa Uingereza na Rais wa Iran tangu Machi, 2021 wakati kiongozi wa zamani wa Uingereza, Boris Johnson alipozungumza na Hassan Rouhani.

Mazungumzo yao ya dakika 30 yanafanyika wakati Uingereza ikitoa taarifa ya pamoja na Marekani, Ufaransa, Italia na Ujerumani kuitaka Iran kukomesha vitisho vyake vya kuishambulia Israel.

Waliitaka Iran "kuacha vitisho vyake vinavyoendelea vya mashambulizi ya kijeshi dhidi ya Israel na kujadili madhara makubwa kwa usalama wa kikanda iwapo shambulio kama hilo litatokea".

Viongozi hao pia walizungumzia suala la kuunga mkono "ulinzi wa Israel dhidi ya uvamizi wa Iran na mashambulizi ya makundi ya kigaidi yanayoungwa mkono na Iran".

BBC.

HABARI ZIMEANDALIWA NA Hamid Yassin

# Wasanii walivyooneshana ubabe Tuzo za 'HAPAWARDS' 2024

REPA wa Bongo Fleva, Profesa Jay ametwaa Tuzo ya Heshima kwenye tuzo HAPAWARDS 2024, zilizofanyika kwenye Ukumbi wa The Super Dome Masaki wikiendi iliyopta.

Profesa Jay aliwaongoza wasanii kadhaa walioibuka kidedea kwenye Tuzo hizo za HAPAWARDS (Hollywood And African Prestigious Awards ) ambazo zimekuwa zikitolewa kwa miaka saba mfululizo nchini Marekani ambapo mwaka huu kwa mara ya kwanza zinafanyika Afrika.

Naye nyota wa filamu nchini, Davina alishinda kwenye kipengele cha msanii aliyewakilisha vizuri kimataifa zinazoandaliwa Marekani kutokana na ushindani uliokuwa kwa washiriki wengine wa kipengele hicho na yeye mwenyewe akizunguza baada ya kutangazwa mshindi mbali ya kushukuru, pia alisema hakutegemea.

Davina alisema, kuwashinda waigizaji kama akina Elizabeth Michael 'Lulu', Johari na Batuli katika kinyang'anyiro hicho, ambao amekiri wote ni wasanii wakali kwenye tasnia ya filamu na pia amefurahia kuona kazi zao zinaonekana na kufuatiliwa hadi Marekani.

Mwigizaji, Welu Sengo ametwaa tuzo ya msanii bora wa kike wa tamthilia kwenye Tuzi hizo za HAPAWARDS 2024, huku Mlimbwende, Flaviana Matata ametwaa Tuzo ya Mwanamitindo bora wa kike Kimataifa.

Naye Sadam Nawanda ametwaa Tuzo msanii bora wa kiume wa Tamthilia kwenye tuzo za mwaka huu, naye Young Lunya amechukua tuzo ya msanii bora wa Hip hop Tanzania.

Nayo Bendi ya Twanga Pepeta katika usiku huo wa Tuzo za 'HAPAWARDS' ilichukua tuzo ya Bendi Bora Tanzania. Twanga Pepeta ilikuwa inashindanishwa na bendi za Malaika, Msondo Ngoma, Sikinde Ngoma ya Ukae na Mjengoni Classic Band.

Mwanamama, Lamata amechukua tuzo ya Muongozaji Bora wa Filamu nchini.



Lamata alikuwa amewashinda waongozaji wengine wa tamthilia ambao ni Vicent Kigosi 'Ray' na William Mtitu.

Bendi ya Jahazi Morden Taarabu haikuwa nyuma katika shindano hilo baada ya kushinda tuzo ya bendi bora ya taarabu. Jahazi Morden Taarabu ilikuwa inashindanishwa na Nakshinakshi, Tamtam, na First Classic.

Tamthilia ya 'Jua Kali' usiku huo ilitwaa tuzo ya Tamthilia Bora huku

msanii wa Singeli Dulla Makabila akishinda tuzo ya msanii bora wa Singeli kwa kuwashinda Meja Kunta na Shoro Mwamba.

Naye Mchekeshaji mahiri nchini, Joti ameshukuru kupata tuzo hizo za Hollywood And African Prestigious Awards kwenye kipengele cha mchekeshaji bora wa mwaka kupitia filamu yake ya komedi ya 'Maharage ya Mbeya'.

Katika hatua nyingine, mwigizaji, Godliver Gordian naye alifanikiwa kushinda tuzo ya msanii bora wa kike wa Filamu Tanzania kwenye Tuzo hizo za HAPAWARDS 2024.

Tuzo za HAPAWARDS (Hollywood And African Prestigious Awards ) zimekuwa zikitolewa kwa miaka saba mfululizo nchini Marekani ambapo kwa mwaka huu kwa mara ya kwanza zinafanyika nchini Tanzania.





## 'Chokoraa': Kuna unafiki mkubwa kwenye muziki wa dansi



MWANAMUZIKI mahiri wa muziki wa dansi nchini, Khalid Chuma 'Chokoraa' amesema, ndani ya muziki huo kuna unafiki mwingi kitu kinachokwamisha kuwapo kwa ushirikiano wa kuupeleka mbele zaidi ya ulipo.

Mtunzi na mwimbaji huyo wa bendi ya Twanga Pepeta International ambaye pia ni bondia wa ngumi za kulipwa, amesema wanamuziki wengi wa dansi ni wanafiki, kiasi watu wanaogopana kushirikiana kwa kuhofia kufanyiwa 'usnichi' na kufanya dansi isidorore.

## Tamasha la Kizimkazi Jumapili

TAMASHA kubwa la utamaduni na ngoma za asili litazinduliwa rasmi wiki ijayo na Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi, Agosti 18 na kufanyika kwa siku saba huko Kizimkazi, visiwani Zanzibar.

Hili ni zaidi ya tamasha! Ndivyo unaweza kutamka wakati tamasha hilo la nne la Kizimkazi likifunguliwa Jumapili ijayo mjini hapa, linatajwa kufungua fursa mbalimbali za kijamii, kimichezo na kiuchumi.

Lilianzishwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan miaka minne iliyopita huko nyumbani kwao Kizimkazi mahali alipozaliwa na kuanza elimu yake ya msingi.



# Wavu ilivyotamatika kibabe mzunguko wa kwanza




**Na Valensi Mbaga**

MZUNGUKO wa kwanza wa ligi ya mpira wa wavu Tanzania haukutamatika kinyonge kwani ilitoa nafasi ya kushuhudia mitanange mikali kati ya timu 10 za wanaume na timu 7 za wanawake zilizofuana katika viwanja vya Mwembeyanga jijini Dar Es Salaam.

Katika mzunguko wa kwanza ilishuhudiwa michezo kabambe huku vilabu mbalimbali viling'ara zaidi na vingine vikiwa na wakati mbaya zaidi kimchezo.

Kwa upande wa wanaume timu zilikuwa katika makundi mawili na vipigo vikubwa vilishuhudiwa katika kundi la kwanza ambapo timu kinara wa kundi High Voltage ya jijini Dar Es Salaam ikizicharaza timu zote zilizopo kwenye kundi A.

Kipigo kikubwa kutoka kwa High Voltage kilienda kwa The Capitals yenye makazi yake pale Jijini Dodoma kwa seti tatu bila (3- 0), pia ikaiadhibu vikali Faru Kv na Bandari zote za jijini Dar es salaam kwa seti tatu kwa moja (3-1) na kuwafanya kuongoza kundi hilo wakiwa na alama 12 katika michezo minne.

Katika kundi B lilisheheni magwiji wa mchezo huu katika michuano mbalimbali ikiwemo Tanzania Prisons ambayo ni bingwa mtetezi wa ligi hiyo ya Dareva, Jeshi Stars, JKT, wageni Chui pamoja na Kigoma Port.

Kundi hili mpaka kukamilika kwa mzunguko wa kwanza limeongozwa na Tanzania Prisons waliofanikiwa kukusanya alama 12 kwa kushinda michezo yote katika mzunguko wa kwanza.

Kwa upande wa kundi A timu ya The Capitals ndio walioshika mkia kwa kupoteza michezo yote na kukubali vichapo vikubwa kutoka kwa High Voltage na Bandari. Kundi B walioburuza mkia ni JKT ambao nao walishindwa kutamba katika mchezo wowote.

Timu za wanawake zilikuwa katika kundi moja huku bingwa wa kihistoria wa michuano ya mashule ya UMISETA na UMITASHUMTA Korosho Queens wakiendelea kutamba na kuziadhibu vikali timu kongwe kama Tanzania Prisons na kuwafanya kuwa kileleni kwenye msimamo wa kundi hilo.

Hali ilikuwa tete zaidi kwa JKT ambao sio tu kwa upande wa wanaume bali pia upande wa wanawake kwani walishindwa hata kukusanya alama moja na walipoteza michezo yote sita waliyocheza katika mzunguko huo wa kwanza huku wakipoteza baadhi ya michezo kwa kanuni.

Mzunguko wa kwanza umeibua nyota hatari zaidi ambao majina yao yameimbwa zaidi kama Jord Edward, Francis Peter Agapiti na Nickson Rwekaza wote wanaokipiga katika timu ya High Voltage, Japhet na Shafii kutoka timu ya Tanzania Prisons na kwa upande wa wanawake ni Wamada Salum, Latifa Seif, Rekha na Vanesa John wote kutoka Korosho Queens kwa pamoja walikuwa wachezaji walioongoza kuzipa timu zao matokeo chanya.

Bado kiu ya mashabiki wengi wa mpira wa wavu ni kuona mzunguko wa pili timu gani zitakuja kufanya mabadiliko na kurudi katika nafasi nzuri zaidi katika msimamo wa kundi husika.

Chachu ya ubora wa timu kama JKT bado inazidi kushika kasi kutokana na nafasi waliyopo mpaka sasa kwa timu zote mbili yaani wanaume na wanawake pia.


Je, timu ya Korosho Queens itaendeleza ubabe wake kwenye mzunguko wa pili baada ya kutoka kushiriki mashindano ya mashule ya Afrika mashariki ( FEASA) na je, wakongwe Tanzania Prisons watakubali kupokea kipigo kingine kutoka kwa Korosho Queens au watarudi wakiwa bora zaidi?

Lakini pia kwa upande wa wanaume tutegemee kuona High Voltage na Tanzania Prisons zikidumisha utawala wake katika makundi yao? Au timu zote zitarudi kupigania na kuchukua kijiti cha kuwa kileleni?




Majibu yote hayo yatapatikana katika mzunguko wa pili utakaoanza Septemba 27 katika viwanja vya Mwembeyanga, Temeke jijini Dar es salaam. Na hapa tutajua nani atamshusha yupi katika nafasi gani kabla ya kwenda katika mzunguko wa tatu wa ligi hiyo.


# Nani ataizuia Man City kutwaa ubingwa tena England?











**LONDON, England**

WAKATI Ligi Kuu England (EPL) inaanza wikiendi hii, swali la kila mwaka ni hili, kuna timu yoyote inayoweza kuizuia Manchester City kuchukua ubingwa?

Kwa msimu wa tisa mfululizo kikosi hicho cha Pep Guardiola kinapewa nafasi kubwa ya kutwaa taji la Ligi Kuu ya England.

Wameshinda mataji sita kati ya saba yaliyopita, yakiwemo manne mfululizo.

Timu saba wapinzani wa City ambazo zina uwezo pia wa kutwaa taji, zinatizamwa kama ndizo zenye ubavu wa kuivua ubingwa Manchester City. Zimepangwa hapa kulingana na nafasi zao za kumaliza msimu uliopita.

### Arsenal

Mwisho wa msimu uliopita, walikuwa nafasi ya pili, pointi mbili chini ya City. Wamemaliza washindi wa pili chini ya City katika misimu miwili iliyopita.

The Gunners wamefanya mabadiliko makubwa, wamemleta mlinzi wa Italia Riccardo Calafiori kutoka Bologna kwa ada ya pauni milioni 42. Anaweza kucheza beki wa kushoto au wa kati.

Pia wamegeuza mkataba wa mkopo kuwa wa kudumu kwa kipa wa Uhispania, David Raya, ambaye alimpiku Aaron Ramsdale na kuwa nambari moja msimu uliopita.

Winga wao Bukayo Saka ndiye mfungaji wao bora katika misimu miwili iliyopita. Na wanahusishwa kutaka kumnunua mshambuliaji wa Napoli, Victor Osimhen.

Nahodha wa Arsenal, Martin Odegaard alisema kwamba, wameibadilisha klabu na anaamini Arsenal watashindania taji kwa muda mrefu.

### Liverpool

Mwisho wa msimu walikuwa nafasi ya tatu, pointi tisa chini ya City. Liverpool wanaanza msimu bila ya meneja Jurgen Klopp kwa mara ya kwanza tangu msimu wa 2015-16.

Klopp alitangaza ataondoka mwishoni mwa msimu, lakini tangazo lake lilikuja katikati ya msimu uliopita na nafasi yake imechukuliwa na Arne Slot mwezi Mei.

Mdachi huyo anaonekana kubadilisha mtindo wa uchezaji wa Liverpool kutoka mchezo wa nguvu na haraka hadi ule wa kumiliki mpira.

Liverpool ndio timu pekee mbali na City kushinda taji la Ligi Kuu katika kipindi cha miaka saba iliyopita, bado hawajasajili mtu yeyote msimu huu, lakini Slot anatumai watasajili.

### Aston Villa

Mwisho wa msimu uliopita walikuwa nafasi ya nne na pointi 23 chini ya City. Ilifuzu Ligi ya Mabingwa kwa kufanikiwa kumaliza katika nafasi ya nne msimu uliopita.

Unai Emery ameigeuza klabu hiyo kutoka kugombea kutoteremka daraja hadi timu ambayo inazungumzwa kama mshindania taji msimu uliopita, na hata bado hajaiongoza angalau kwa miaka miwili.

Klabu hiyo inalazimika kuuza wachezaji msimu huu wa joto ili kutimiza kanuni za faida na kifedha za Ligi Kuu ya Uingereza.

### Tottenham Hotspur

Mwisho wa msimu uliopita walikuwa watano, wakiwa chini ya City kwa alama 25. Walianza vyema msimu uliopita chini ya Ange Postecoglou na walikuwa nyuma kwa pointi tano kileleni baada ya mechi 10.

Archie Gray, pauni milioni 30 kutoka Leeds, Lucas Bergvall pauni milioni 8.5 kutoka Djurgarden na George Feeney kutoka Glentoran - aliyesajiliwa kwa timu ya vijana chini ya umri wa miaka 18, ndio pekee waliosajiliwa majira ya joto hadi sasa.

Winga chipukizi wa Korea Kusini, Yang Min-hyuk atajiunga na kikosi hicho mwezi Januari.

Mikey Moore, mshambuliaji wa akademi mwenye umri wa miaka 16, amevutia katika mechi za kirafiki za kabla ya msimu mpya.

### Chelsea

Mwisho wa msimu uliopita ilishika nafasi ya sita na alama 28 chini ya City. Kocha Enzo Maresca, baada ya kuifundisha Leicester na kupanda daraja, alichukua nafasi ya Mauricio Pochettino katika kiti moto cha The Blues.

Wamesajili wachezaji wengi majira ya kiangazi kama vile Kiernan Dewsbury toka Hall, Tosin Adarabioyo na Omari Kellyman wote wana uzoefu wa Ligi Kuu.

Beki mkongwe wa kati Thiago Silva, pamoja na Hakim Ziyech, Ian Maatsen, Lewis Hall na Omari Hutchinson wote walikuwa nje kwa mkopo msimu uliopita na sasa wameondoka moja kwa moja. Na Conor Gallagher anatarajiwa kuhamia Atletico Madrid.

### Newcastle United

Mwisho wa msimu uliopita ilishika nafasi ya saba na pointi 31 chini ya City. Newcastle walifanya vyema msimu wa 2022/23 kwa kufuzu Ligi ya Mabingwa, lakini kumaliza katika nafasi ya saba msimu uliopita kulionekana kama kushuka chini.

Sasa Newcastle wanatumai watambakiza meneja Eddie Howe, ambaye anapendekezwa kuwa kocha wa England.

Habari njema ni Alexander Isak, Bruno Guimaraes na Anthony Gordon wote bado wako kwenye klabu."

### Manchester United

Mwisho wa msimu walikuwa nafasi ya nane na pointi 31 chini ya City. Walimaliza vibaya zaidi tangu ligi ya msimu wa 1989/90, walipomaliza katika nafasi ya nane – ingawa msimu huu wameshinda Kombe la FA.


Meneja Erik ten Hag alitarajiwa kupoteza kibarua chake, lakini United waliamua kubaki na Mholanzi huyo ambaye ameshinda mataji katika misimu yake yote miwili klabuni hapo.

Manchester United wametumia pesa kununu vijana wawili msimu huu, mshambuliaji wa Bologna, Joshua Zirkzee kwa pauni milioni 36.5 na mlinzi wa kati wa Lille, Leny Yoro kwa pauni 52.

Hata hivyo, tayari Yoro amejeruhiwa na huenda akakaa nje ya uwanja kwa miezi mingi. Vilevile, wachezaji kadhaa wameondoka kwa uhamisho wa bure akiwemo mchezaji wa zamani wa kimataifa wa Ufaransa, Raphael Varane na Anthony Martial.



## Kona ya Urembo



# Urembo wa kucha kwa mwanamke

**Na Unosye Atufigwege**

UREMBO wa kucha kwa mwanamke umekuwa sehemu muhimu ya mitindo na utamaduni wa urembo kwa karne nyingi. Kucha ni mchakato wa kupamba kucha kwa kutumia rangi, mapambo, na mbinu nyingine za urembo, na umejikita katika nyanja za mitindo, sanaa, na afya ya urembo.

Hapa tutachunguza jinsi urembo wa kucha unavyoathiri maisha ya mwanamke, maana yake katika jamii, na umuhimu wake katika kujitambua na kujiamini.

### Historia na maendeleo ya urembo wa kucha

Kucha zimekuwa sehemu ya mapambo ya mwanamke kwa muda mrefu, zikionyesha mtindo, hali ya kiuchumi, na hadhi ya kijamii. Katika misimu ya zamani, wanawake walitumia mbinu za asili kupamba kucha zao kwa kutumia rangi za mimea, madini, na nyenzo nyingine za asili.

Kwa mfano, katika Misri ya Kale, wanawake walitumia hina, ambayo ni rangi ya mimea, kupamba kucha zao na kutoa ishara ya uzuri na hadhi. Katika utamaduni wa Kichina, alama za kucha ndefu zilitumika kuonyesha hadhi na utajiri wa mwanamke.

Kwa karne za hivi karibuni, maendeleo ya teknolojia ya urembo yameleta mapinduzi makubwa katika mbinu za urembo wa kucha. Kutoka kwa kucha za kawaida hadi kucha za gundi, rangi za gundi, na mapambo ya mitindo ya juu, wanawake sasa wana chaguo nyingi za kuboresha urembo wao. Ukitazama taswira za sasa, unaweza kuona matumizi ya vidokezo vya kisasa kama vile gundi za kucha, uchoraji wa sanamu za kucha, na vifaa vya kuboresha umbo na mwonekano wa kucha.

### Urembo wa Kucha na maendeleo ya kijamii

Urembo wa kucha sio tu kuhusu mtindo, bali pia unachangia katika maendeleo ya kijamii na kiuchumi. Kwa wanawake, ukiangalia vizuri ni sehemu ya kujenga hali ya kujiamini na kujistahi.

Kwa mfano, matokeo ya tafiti yanaonyesha kuwa wanawake wanaotunza vizuri kucha zao wanajihisi kuwa na kujitambua zaidi na kujiamini zaidi katika mazungumzo ya kijamii na kitaaluma.

Pia urembo wa kucha unasaidia kuongeza hali ya kujistahi, na hivyo kuchangia katika maendeleo ya kijamii ya mwanamke.

Urembo wa kucha pia unaweza kuwa na athari chanya katika tasnia ya urembo. Wafanyabiashara wa bidhaa za urembo wa kucha, ikiwa ni pamoja na vishikizo vya kucha, rangi, na mapambo, wanatoa nafasi za ajira na kuimarisha uchumi kwa walimbwende.

Urembo wa kucha pia unajenga taswira ya kipekee katika tasnia ya mitindo, na wanawake wengi wanapata fursa ya kuonyesha ubunifu wao kupitia mapambo haya.

### Utunzaji wa kucha

Utunzaji wa kucha unajumuisha hatua mbalimbali ambazo zinaweza kuhakikisha kwamba kucha zinabaki kuwa na afya na kuonekana vizuri.

Kwanza, ni muhimu kuhakikisha usafi wa kucha kwa kusafisha mara kwa mara na kuondoa uchafu na mabaki ya mapambo. Kusafisha kucha kwa kutumia sabuni ya laini na maji ni hatua ya msingi, lakini ni muhimu pia kutumia bidhaa maalum za kuondoa rangi kama vile viondoa gundi ili kuepuka madhara ya ziada kwa kucha.

Pili, matumizi ya mafuta ya kucha na krimu za kulainisha ni muhimu kwa kuboresha uimara na unyevu wa kucha. Mafuta ya kucha yanaweza kupunguza ukavu na kupunguza hatari ya kucha kuvunjika.

Aidha, matumizi ya virutubisho vya afya kama vile vitamini E na omega-3 vinaweza kusaidia kuboresha afya ya kucha na ngozi inayozunguka.

Tatu, ni muhimu kuepuka matumizi ya bidhaa zenye kemikali kali kama vile baadhi ya rangi za kucha na viondoa gundi. Bidhaa hizi zinaweza kuathiri afya ya kucha kwa kuvunja kinga yao ya asili na kusababisha ukavu au uharibifu wa kucha.

Kucha za kubandika, ingawa zinatoa urahisi na mitindo, zinaweza kuwa na athari mbalimbali kiafya ikiwa hazitumiki au kutunzwa vizuri. Hapa kuna baadhi ya athari zinazoweza kutokea:

### Maambukizi ya Ngozi

Kuchochea Maambukizi, ikiwa kucha za kubandika zimejificha au zinaambatana na ngozi kwa muda mrefu, zinaweza kuwa na mazingira bora kwa bakteria na fangasi. Hii inaweza kusababisha maambukizi kama vile ya ngozi au fangasi kwenye ngozi inayozunguka kucha.

### Madhara kwa kucha halisi

Kuvunjika kwa kucha, kucha za kubandika zinaweza kusababisha kucha halisi kuwa na mifumo ya kuvunjika au kupasuka, hasa kama zinashikiliwa kwa nguvu au ikiwa zimeondolewa kwa njia mbaya. Hii inaweza kuathiri afya ya kucha ya asili.

### Uathiri wa Kemikali

Baadhi ya kucha za kubandika zinaweza kuwa na viambato vya kemikali kama vile 'formaldehyde' au plastiki ambazo zinaweza kuathiri afya ya kucha na ngozi. Kemikali hizi zinaweza kusababisha ukavu, mzio, au athari nyingine kwa ngozi.

### Madhara kwa Mwonekano wa Kucha

Madhara ya Muda Mrefu: Ikiwa kucha za kubandika zinaachwa kwa muda mrefu bila kuondolewa, zinaweza kuathiri mwonekano wa kucha halisi kwa kuacha alama au kuharibu uso wa kucha. Hii inaweza kuhitaji matengenezo au huduma ya kitaalamu kwa ajili ya kurekebisha.



### Matatizo ya kifaa cha kucha

Vifaa vya kubandika, ikiwa vifaa vya kucha za kubandika vinavyotumika havina usafi, vinaweza kuwa na bakteria au vimelea vingine ambavyo vinaweza kuathiri afya ya kucha na ngozi.

### Madhara ya Uondoaji

Uondoaji mbaya, kuondoa kucha za kubandika kwa kutumia mbinu zisizo sahihi au viondoa gundi zenye kemikali kali kunaweza kusababisha uharibifu wa kucha ya asili au ngozi inayozunguka. Hii inaweza kuwa na athari kama vile ngozi kuvimba au kucha kuathirika.

### Vidokezo vya kuepuka athari



1. Tumia Bidhaa Zilizojaribiwa
Chagua kucha za kubandika kutoka kwa watengenezaji wenye sifa nzuri na viambato salama.

2. Hakikisha Usafi
Tumia vifaa safi na usafi wa ngozi unavyoyowezekana ili kupunguza hatari ya maambukizi.

3. Epuka matumizi ya muda mrefu usiache kucha za kubandika kwa muda mrefu bila kupumzika kwa kucha zako ili kuepuka madhara ya muda mrefu kwa afya ya kucha.

4. Fuata Maagizo ya Matumizi
Fuata maagizo ya mtengenezaji kuhusu matumizi na uondoaji wa kucha za kubandika ili kuepuka athari za kiafya.



Kwa kuzingatia vidokezo hivi, unaweza kupunguza hatari na kuhakikisha matumizi salama ya kucha za kubandika.

### Hitimisho

Urembo wa kucha kwa mwanamke ni kipande cha kipekee cha utamaduni na mitindo ambayo ina athari kubwa katika maisha ya mwanamke. Inachangia katika kujitambua, kujiamini, na kuboresha hali ya maisha ya kila siku.

Kwa kuzingatia maendeleo ya teknolojia na mitindo, urembo wa kucha utaendelea kubadilika na kuleta mawazo mapya, huku ukifunga maandiko ya kijamii na kiutamaduni.

Kwa hivyo, urembo wa kucha ni sehemu muhimu ya maisha ya mwanamke na utamaduni wa kisasa, ukionyesha uzuri, ubunifu, na hadhi ya kijamii.

# Wanariadha Congo DR waingia 'mitini' Ufaransa

**PARIS, Ufaransa**

WAKATI sherehe za kufunga michezo ya Olimpiki zikifanyika mjini Paris, imebainika wanariadha watatu wa DR Congo wametoweka kambini kwao tangu Jumapili, siku ya mwisho ya michezo hiyo ya 33.

Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo ilishiriki katika matukio manne judo, kuogelea, riadha na ngumi huku nchi hiyo ikikumbwa na ushiriki duni na kumaliza mashindano bila kutwaa medali.

Wakongo waliofanya vizuri ni Dominique Lasconi aliyetolewa katika raundi ya kwanza katika mbio za mita 100 kwa wanaume akimaliza katika nafasi ya 7 baada ya kufanikiwa kumaliza wa tatu katika awamu ya awali kwa muda wa sekunde 10 na nukta 54.

Leo yetu ndiyo kesho yetu
Uelekeo Spoti
| Jumatano Agosti 14-20, 2024 |



# Simba yamnasa Leonel Ateba

**Na Mwandishi Wetu**

## ● Kuwa kinara wa mashambulizi Msimbazi

SIMBA SC imekamilisha usajili wa mshambuliaji Leonel Ateba raia wa Cameroon kwa mkataba wa miaka miwili wenye kipengele cha kuongeza mwaka mmoja akitokea USM Alger ya nchini Algeria.

Habari kutoka ndani ya Simba zimedai kuwa, Ateba ni pendekezo la kocha wao Fadlu Davids na huenda akachukua nafasi ya kipa wao Mmorocco, Ayoub Lakred ambaye anatolewa kwenye mfumo wa usajili.

Mchezaji huyo atapokea mshahara wa dola 8,000 na wenye kipengele cha kuongezeka mshahara wake kama atafunga bao 15 au kufunga bao 10 na 'assisti' 5 katika msimu wake wa kwanza na mshahara wake utafika hadi dola 9,000.

Kwa sasa klabu ya Simba SC inaendelea kukamilisha baadhi ya vipengele kwenye mfumo wa TMS ili waweze kukamilisha usajili huo na kumtangaza rasmi kwa mashabiki na wanachama wake.

Mkataba wa mchezaji huyo umeanza rasmi Agosti 10, 2024.

Chanzo chetu kimefafanua kuwa, wakati kocha Fadlu alipohitaji mshambuliaji mpya, viongozi wa Simba wakapendekeza asajiliwe Ricky Banda kutoka Red Arrows ya Malawi, lakini baadaye Mchambuzi wa video wa klabu hiyo, Mueez Kajee, akajiridhisha Banda hawezi kufiti katika mfumo wa uchezaji wa Fadlu.




Simba walitaka kumpa kocha wao kitu chochote anachotaka ili wakija kumdai mafanikio asiwe na visingizio, wakamwambia zimebaki siku chache sana dirisha la usajili kufungwa na muda wa kutafuta mchezaji ni mchache hivyo kama kuna straika anamfahamu anayecheza anavyotaka basi aweke jina mezani wapambane kumpata.

Inaelezwa kocha Fadlu akapendekeza majina mawili, moja ni mshambuliaji raia wa Ethiopia anayekipiga Mamelodi Sundowns ya Afrika Kusini, Abubekir Nessir na mwingine ni Straika wa USM Alger raia wa Cameroon, Leonel Ateba.

Baada ya kuwafuatilia wote hawa, Simba wakabaini kuna urahisi zaidi kumpata Nessir kutoka Mamelodi kwa sababu hana nafasi ya kucheza pale lakini wakagundua pia mchezaji huyo ni mtu wa majeraha ya mara kwa mara hivyo hawezi kuisaidia timu muda mrefu.

Hivyo, Simba wakajitosa moja kwa moja kukamilisha uhamisho wa Ateba, mwanzo 'dili' hilo lilikua gumu kwa sababu USM Alger hawakuwa tayari kumuuza lakini likaingia wepesi baada ya Ateba mwenyewe kuwaomba mabosi wa klabu yake wamuuze akapate nafasi ya kucheza zaidi

Kwa nini Ateba aliomba kuondoka USM Alger? Sababu ni hii, mchezaji huyo kiasili ni mshambuliaji wa kati lakini USM Alger alikua anatumika kama winga na mara nyingine kama namba 10 nyuma ya Straika anayeanza katika kikosi cha Waarabu hao ambaye ni Abdoulaye Kanu raia wa Mali.

Hii ndio maana ukitazama takwimu za Ateba katika mechi 16 ana pasi za magoli nyingi zaidi (8) na kufunga goli moja pekee.

Simba SC wamekubali kulipa shilingi za Kitanzania milioni 523 kwa USM Alger ili wapate hitaji la kocha wao na hatimaye 'dili' hilo limekamilika.

**Na Mwandishi Wetu**

# Yanga, Azam FC macho Klabu Bingwa Afrika

WAWAKILISHI wa Tanzania Bara kwenye michuano ya Klabu Bingwa Afrika, Yanga na Azam FC baada ya kumalizana kwenye fainali ya Ngao ya Jamii, sasa macho yao yote wameyaelekeza kwenye mashindano hayo yanayoanza wikiendi hii.

Meneja wa Habari na Mawasiliano wa klabu ya Yanga, Ally Kamwe amenena kuwa, tayari kikosi chao kimeanza mazoezi ikiwa ni mawindo maalumu dhidi ya Vital'O FC ya Burundi Jumamosi hii kwenye Uwanja wa Azam Complex.

Kamwe amejinasibu kuwa, wanataka kutumia mechi hiyo ya kwanza ya Jumamosi kufuzu michuano hiyo ya ngazi ya awali ya Klabu Bingwa Afrika kisha ile mechi ya marudiano ya Agosti 24 itakuwa ya kukamilisha ratiba na kuwafurahisha mashabiki.

"Hii mechi ya Jumamosi tutakuwa ugenini pale Chamazi, tunataka kuwafunga magoli mengi ya kutosha ili tuimalize kabisa mechi, halafu ile ya marudiano pale Uwanja wa Mkapa iwe ya kucheza soka la kuwafurahisha mashabiki wetu," ametamba Kamwe.

Kamwe amewasihi mashabiki wao kujitokeza kwa wingi Jumamosi kuwapa shime ya ushindi wachezaji wao, kwani kocha wao Miguel Gamondi atakuwa ameshatimiza wajibu wake na pale uwanjani itabaki kazi ya wachezaji na mashabiki pekee.

Naye kocha wa Vital'o FC, Sahabo Parris ametamba kuwa, watawashangaza wadau wa soka wanaoamini watapigwa kipigo cha paka mwizi na Yanga katika mechi hiyo ya Jumamosi.

Sahabo amedai kuwa, baada ya kuwatizama Yanga walipocheza na watani wao Simba kwenye pambano la nusu fainali ya Ngao ya Jamii, ameona mianya mingi ya kuwamaliza wapinzani wao bila shak yoyote ile.

"Yanga wana kasi kubwa wanapoelekea lango la adui, lakini ukiwadhibiti wasikufunge na ukajibu kwa haraka mashambulizi yao upo uwezekano mkubwa wa kuwafunga," amedai Saahabo.

Wakati Yanga wakikaribishwa na Vital'O Jumamosi pale Azam Complex, siku moja baadaye uwanja huo utakuwa na mechi ya kukata na shoka baina ya wenyeji Azam FC na APR FC ya Rwanda.

Azam FC baada ya kushiriki Kombe la Shirikisho kwa miaka mingi mfululizo, hatimaye msimu huu wamerejea kwa mara ya pili kwenye michuano ya Klabu Bingwa Afrika nao pia wanataka kuitumia mechi ya Jumapili kushinda kwa idadi kubwa ya magoli ili kujijengea mazingira mazuri ya kusonga mbele mzunguko wa pili.

Msemaji wa klabu hiyo, Hashim Ibwe amewaomba mashabiki wao kujitokeza kwa wingi pale Chamazi Complex ili kuimaliza hiyo mechi hapa hapa nyumbani, kwani APR huwa wagumu sana wanapokuwa kwao.

